# IKULU ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 020 ISSN 1821 - 8253 MACHI - APRILI 2015



# SMZ inavyoliimarisha zao la mwani

- Wakulima wanautumia kutengenezea bidhaa mbali mbali

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu**
Hassan K. Hassan

**Mhariri Msaidizi**
Ali S. Hafidh

**Waandishi**
Said J.Ameir
Rajab Y. Mkasaba
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

**Mpiga Picha**
Ramadhan O. Abdalla

**Msanifu**
Aziz I. Suwed


## UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.


Jarida hili limetolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

P.O.BOX: 2422

Zanzibar - Tanzania

Phone: +255 223 081/5

Fax: 024 223 3722

Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz


# Maoni ya Mhariri

## Tuwekezeni wenyewe kwa kutumia rasilimali tulizonazo

Mazingira au mwenendo wa kibiashara duniani kote humlazimisha kila mfanyabiashara kutumia njia zozote zitakazomhakikishia kuwa anatumia gharama ndogo kwa kadri itakavyowezekana ili hatimaye aweze kupata faida kubwa zaidi.

Zanzibar kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeona umuhimu wa kuwashajiisha wafanyabiashara na kwa muda mrefu imekuwa ikichukua juhudi maalum kutangaza fursa za uwekezaji sambamba na kuwashawishi wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza Zanzibar kwa faida ya wawekezaji na Serikali kwa jumla.

Maeneo yenye kuhitaji kuwekezwa Zanzibar na kupatikana faida ni mengi, lakini kwa muda mrefu mkazo uliwekwa katika kuyatangaza maeneo ya utalii, uvuvi wa bahari kuu, viwanda na kilimo. Hata hivyo, utalii hasa katika ujenzi wa hoteli ndilo eneo pekee lililowavuta wawekezaji wengi.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Fedha Zanzibar, idadi ya watalii wanaokuja kutembelea Zanzibar imeongezeka kutoka watalii 132,836 mwaka 2010 na kufikia watalii 274,619 mwaka 2014. Ni dhahiri, uwekezaji katika sekta hiyo umeonekana kuwa na faida kubwa, lakini unatokana na mazingira mazuri kijiografia, fukwe mwanana za kuvutia, na bila ya shaka hali ya amani na utulivu, mambo ambayo Serikali imekuwa ikifanya kila juhudi kuyalinda na kuyadumisha.

Lakini ni ukweli uliowazi kwamba uwekezaji katika sekta nyengine ambazo nazo zinaweza kuleta faida kubwa hasa sekta za kijamii, ambazo vile vile zinaambatana na masuala ya utalii bado hazijatangazwa vizuri na hivyo uwekezaji wake haujaonekana kushika kasi kama ilivyo ujenzi wa hoteli za kitalii.

Serikali imetambua kuwa uwekezaji mkubwa katika sekta nyengine za kijamii kama vile sekta ya afya, unahitaji kuwekewa vivutio maalum ambavyo siyo tu vitaishia kwenye sekta hiyo, lakini vile vile vitawezesha kuwavutia wawekezaji wengine wa ndani na nje katika sekta nyengine ambazo uwekezaji wake haujaleta tija kubwa katika uchumi na wananchi wa Zanzibar.

Miongoni mwa maeneo muhimu ambayo yanaweza kuleta tija kubwa kwa jamii na ambayo ni sehemu ya utalii lakini bado hayajashughulikiwa ipasavyo, ni utalii wa kimikutano "conference tourism", utalii wa kimichezo "sports tourism" na utalii wa afya "health tourism".

Kwa upande wa sekta ya kilimo na uvuvi, vile vile zipo fursa kadhaa za uwekezaji wa kilimo cha mboga mboga kwa ajili ya soko la utalii. Kilimo cha mazao ya baharini kinaweza kunufaisha soko la ndani na soko la nje, ambapo uvuvi wa bahari kuu utaleta tija zaidi kwa suala la ajira na usafirishaji wa samaki nje ya nchi.


Kutokana na kutambua umuhimu wa uwekezaji na fursa zilizopo, Serikali imekamilisha Mpango Mkuu wa Uendelezwaji wa Maeneo Huru yaliyoko Fumba na kwamba tayari ipo baadhi ya miradi inayoendelezwa.

Sambamba na hatua hiyo, Serikali imeimarisha mazingira ya uwekezaji ambapo hivi sasa huduma za vibali vya kazi na ukaazi kwa wawekezaji zinapatikana ndani ya siku 14 kinyume na ilivyokuwa hapo kabla.

Pamoja na juhudi kubwa ambazo Serikali imekuwa ikichukua, muamko wa wawekezaji wa ndani katika kuzitumia ipasavyo fursa zilizopo bado ni mdogo, jambo ambalo siyo tu halitoi taswira nzuri ya kuwa na uchumi endelevu unaomilikiwa na wazalendo, lakini vile vile mwenendo huo unapelekea kuifanya Zanzibar kuendelea kuagiza vitu vingi nje ya nchi hata vile ambavyo vinaweza kuzalishwa hapa hapa Zanzibar.

Wakati tukiendelea kushajiisha na kusubiri wawekezaji kutoka nje ya nchi, wakati umefika sasa kwa wazalendo kuanza kuwekeza kwa kasi kubwa kwa kutumia rasilimali tulizonazo.

Tunapaswa kuyatumia mazingira mazuri yaliyopo kwa kujivunia mafanikio ya jitihada za Serikali katika kuimarisha miundombinu ya barabara, maji safi na salama na umeme wa uhakika, mambo ambayo yanatoa fursa pana zaidi ya kuwekeza katika sekta zote muhimu.



# SMZ inavyoliimarisha zao la mwani

## • Wakulima wanautumia kutengenezea bidhaa mbali mbali



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimkabidhi Kihori Bw. Kombo Salim Hamadi mkulima wa mwani wa Tumbe Magharibi, Mkoa wa Kaskazini Pemba wakati wa sherehe za kukabidhi vihori kwa wakulima wa mwani zilizofanyika katika ukumbi wa Salama katika Hoteli ya Bwawani Mjini Unguja tarehe 9 Machi 2015*

Kilimo cha mwani Zanzibar ni moja kati ya shughuli muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar ikizingatiwa kuwa, hivi sasa kilimo hicho kinaajiri zaidi ya watu 20,000 wengi wao wakiwa wanawake wa vijijini, na ni zao la pili kati ya mazao yanayosafirishwa kwa wingi nchi za nje hapa Zanzibar.

Hatua hiyo inatosha kudhihirisha kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahitaji kuchukua kila aina ya juhudi katika kuimarisha uzalishaji wa zao hilo, ili liweze kuwa na tija zaidi kwa wakulima na pia katika kuchangia Pato la Taifa.

Juhudi za Serikali katika kuimarisha zao la mwani na mazao mengine ya biashara kwa wananchi zimekuwa zikionekana wazi wazi katika matukio tofauti, kutokana na ukweli kwamba harakati hizo zinakwenda sambamba na jukumu la kuwaunga mkono wananchi kwa kuwajengea uwezo wa kuimarisha miradi yao kwa kuongeza uzalishaji na kuongeza kipato chao, kama ilivyoelezwa kwenye Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 – 2010. Ilani hiyo imekuwa ikitekelezwa kwa ufanisi mkubwa ndani ya kipindi hiki cha zaidi ya miaka minne sasa.

Katika hotuba yake ya Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 51 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alibainisha kuwa idadi ya tani za mwani zilizozalishwa katika kipindi cha miaka minne tokea alipokabidhiwa madaraka ya Urais ni jumla ya tani 51,687 zenye thamani ya TZS bilioni 18.7 zote zikiwa zimesafirishwa nje ya nchi katika kipindi hicho.

"Zao hili hivi sasa limekuwa ni miongoni mwa mazao makuu ya biashara tunayosafirisha nje ya nchi. Hili ni zao la pili kwa kusafirishwa nje baada ya karafuu. Habari njema ni kuwa mwani tunaozalisha Zanzibar unasifika kwa ubora duniani".



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia bidhaa zilizotengenezwa na kikundi cha Ulezi ni Kazi cha Shehia ya Fujoni Jimbo la Kitope kwa kutumia zao la mwani wakati wa sherehe za kukabidhi Vihori kwa wakulima wa mwani tarehe 9 Machi 2015*

Alisema Dk. Shein.

Kimsingi, ugawaji wa vihori au boti ndogo za kuchukulia mwani kwa wakulima wa Zanzibar wanaojishughulisha na kilimo hichi, ni sehemu ya juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuwawezesha kiuchumi wananchi wake. Vihori hivyo vya kisasa vitawapa ahueni wakulima wa mwani, hususan wanawake, ambao mara nyingi wamekuwa wakibeba mwani masafa marefu kwa kichwa kuleta ufukweni kwa ajili ya kukausha. Hivyo, vihori hivi vitasaidia kuondoa tatizo hilo na vitatoa msukumo katika kuongeza kiwango cha uzalishaji na bila ya shaka kuongeza kipato cha wakulima.

Aidha, ni dhamira ya Serikali kuona kuwa uwezo wa wananchi katika kubuni mambo mbali mbali kwa kutumia rasilimali zilizowazunguka unaongezeka, ili hatimaye waweze kujikwamua kiuchumi na kufikia malengo waliyojiwekea wao wenyewe na yale yaliyowekwa na taifa.


Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inafahamu kilio kikubwa cha wakulima wa mwani kuwa ni bei. Bei wanayolipwa wakulima wa zao hilo bado ni ndogo na hailingani na kazi kubwa ya uzashaji wanayoifanya. Aidha, SMZ inafahamu changamoto iliyopo ya ukosefu wa vitendea kazi mbali mbali ambavyo vingerahisisha shughuli za wakulima wa mwani. Ni dhahiri, changamoto hizo zinahitaji kufanyiwa kazi, ili kuongeza ubora na kiwango cha uzalishaji wa mwani, na hivyo kuongeza kipato cha wakulima.

Katika jitihada za kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo, Serikali kwa mashirikiano na Shirika la Kimataifa la Huduma za Kujitolea (Voluntary Services Overseas – VSO) na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) imenunua vihori, ili kurahisisha kazi ya ubebaji mwani kutoka baharini kupeleka ufukweni. Vihori hivyo ni vya mwanzo kuwahi kutolewa kwa wakulima wa mwani katika ukanda huu wa Afrika ya Mashariki.

Vihori hivyo ambavyo vimekabidhiwa kwa wakulima ambao tayari wamefanyiwa uchambuzi na kufikia viwango ama sifa zinazohitajika, vimetolewa kwa utaratibu wa mkopo kwa mtu mmoja mmoja na vikundi vya ushirika, kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Fedha zitakazokusanywa katika marejesho ya mikopo hii, zitawawezesha kununua vihori vyengine ambavyo watapatiwa wakulima wengine wa mwani.

Kwa upande mwengine Serikali itahakikisha kuwa bei wanazolipwa wakulima kwa mazao wanayozalisha inalingana na jitihada zao na inawiana na bei ya bidhaa hizo katika masoko ya nje kwa yale mazao ya biashara, kwa kujua kwamba hiyo ndiyo njia bora zaidi ya kuwahamasisha na kuwazidisha ari ya uzalishaji wakulima wote waliopo nchini. Mfano wa jitihada hizo umeonekana kwa upande wa zao la karafuu ambao utaendelezwa kwa mazao mengine.

Akizungumza kwenye hafla hiyo mara baada ya kukabidhi vihori hivyo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliziagiza Wizara za Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH)



kwa ajili ya kufanya utatifi juu ya njia bora za kuzalisha zao hili ikiwa ni pamoja na kuwatafutia wakulima mbegu bora za mwani kutokana na mazingira ya Zanzibar na mahitaji yaliyopo katika soko la nje.

Aidha, Mheshimiwa Rais alishauri utafiti huo uelekezwe katika kukuza ubunifu na mbinu za kusarifu zao hili ili wakulima waweze kutengeneza bidhaa mbali mbali watakazoweza kuuza ndani na nje ya nchi badala ya kuuza mwani kama ni mali ghafi.

Vile vile aliiagiza Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kufanya kazi kwa karibu na wakulima wa mwani kwa lengo la kuhakikisha kuwa bei wanayolipwa wakulima inalingana na hali halisi ya bei ya bidhaa hii katika soko la nje. Aidha, Wizara iongeze kasi katika kutafuta masoko mapya na isitosheke na masoko yaliyopo.

Kwa upande mwengine Serikali inaendelea kuchukua jitihada mbali mbali kuzifanyia kazi changamoto zinazowakabili wakulima wa mazao mengine ya biashara na chakula. Utoaji wa ruzuku pembejeo hasa kwa zao la mpunga ni kielelezo cha jitihada hizo za Serikali.

Kadhalika, Serikali inaendelea na vita dhidi ya wizi wa mazao na mifugo, huku ikiwa imejidhatiti kupambana na wadudu waharibifu wa matunda, pamoja na kufufua mfumo wa zamani wa kuwa na masoko katika miji na vijiji mbali mbali ili wakulima na wavuvi wawe na sehemu bora na za uhakika za kuuzia bidhaa zao. Lengo la jitihada hizi ni kuhakisha kuwa jasho la mkulima linamnufaisha mkulima mwenyewe.

Kwa hatua hii wakulima wa mwani na wananchi wote kwa jumla hawana budi kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuimarisha uzalishaji mwani na mazao mengine ya biashara na chakula na kuwawezesha kiuchumi wananchi wake kwa njia mbali mbali.




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifungua pazia kuashiria ufunguzi wa Hoteli ya Park Hyatt Zanzibar iliyopo Mambo Msiige Mji Mkongwe wa Zanzibar. Kulia kwa Mhe. Rais ni Kaimu Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini. Katikati ni Mmiliki wa Hoteli hiyo Sheikh Ali Sayeed Albawardy*

# Sekta ya Utalii inavyozidi kustawi Zanzibar

Uzinduzi wa hoteli ya nyota tano ya Park Hyatt Zanzibar ndani ya Mji Mkongwe wa Zanzibar wenye hadhi ya urithi wa kimataifa tarehe 8 Machi 2015, kwa mara nyengine tena umethibitisha mafanikio ya utekelezaji wa sera na mipango ya serikali katika kuimarisha sekta ya utalii Zanzibar ambayo ni sekta kiongozi katika ukuaji wa uchumi.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa pamoja na kuwa Zanzibar ina historia kubwa katika mambo mbali mbali ya kuvutia wageni na mazingira ya kuvutia, sekta ya utalii kabla ya Mapinduzi haikuwa imepewa umuhimu uliostahiki na ilitumiwa kwa ajili ya kunufaisha kundi la wachache hasa waliokuwa wakimiliki hoteli chache na nyumba za kulala wageni.

Kabla ya Mapinduzi, Zanzibar ilikuwa na hoteli mbili tu, ambazo ni Zanzibar Hotel na English Club, ambayo sasa ni Africa House. Mara tu baada ya Mapinduzi, Serikali ilianza kuipa sekta hii umuhimu unaostahili kwa kufanya mageuzi ya uendeshaji katika hoteli hizo kwa lengo la kuziimarisha.

Mipango ya Serikali ya kujenga hoteli za kisasa na kuifanya sekta ya utalii kuwa ni sehemu muhimu kwa uchumi na utamaduni wa watu wa Zanzibar ilipangwa na kuanza kutolewa mara tu baada ya Mapinduzi. Katika mwaka 1970 Serikali ilijenga hoteli mpya katika eneo la Funguni na kuitwa Hoteli ya Bwawani, ambayo ilifunguliwa rasmi mwaka 1974 na kuwa moja miongoni mwa hoteli bora zilizoko katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Aidha, Hoteli ya Uwanja wa Amaan nayo ilijengwa katika eneo la Uwanja wa michezo wa Amaan. Kwa upande wa Pemba hoteli nyengine zilijengwa katika mji wa Wete, Chake Chake na Mkoani. Ni dhahiri, kumalizika kwa hoteli hizo kuliongeza kasi ya utalii hapa Zanzibar.





Kadhalika, Shirika la Utalii lililojulikana kwa jina la "Tanzania Friendship Tourist Bureau" (TFTB) nalo liliimarishwa kwa kupatiwa vifaa, nyenzo na vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuwatembeza watalii. Shirika hilo lilifanya juhudi za kuwasomesha wafanyakazi wake kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kusimamia mabadiliko yaliyokuwa yamepangwa katika kuiendesha sekta hiyo.

Baada ya kuanguka kwa bei ya zao la karafuu katika miaka ya thamanini na kudumu hadi mwazoni mwa mwaka 2010, Serikali iliongeza kasi ya kuimarisha sekta ya utalii ili kupunguza utegemezi wa zao hilo na athari za kiuchumi zilizosababishwa na kuanguka kwa bei yake.

Idadi ya watalii ilianza kuongezeka mwaka hadi mwaka kutoka wastani wa watalii 10,000 katika miaka ya 70 hadi kufikia watalii 29,211 mwaka 1986.

Ili kuimarisha zaidi sekta ya utalii, Serikali ilichukua hatua mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuipa nguvu Kamisheni ya Utalii katika kusimamia sekta ya utalii na kupitisha Sheria Nam. 9. Hatua hiyo ilipelekea kuimarika kwa sekta ya utalii ambapo kwa mujibu wa taarifa rasmi za Serikali, sekta ya utalii sasa inachangia asilimia 27 ya Pato la Taifa na kuipatia Serikali asilimia 80 ya fedha za kigeni.

Juhudi nyengine zilizochukuliwa na Serikali katika kuimarisha sekta ya utalii ni kutangaza rasmi dhana ya Utalii kwa Wote tarehe 16 Oktoba, 2011. Lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kuwa kila mwananchi ananufaika na matunda ya utalii na anashiriki katika kuuendeleza utalii.

Sheria ya Utalii Nam. 6 ya mwaka 2009 ambayo imeifuta Sheria Nam. 9 ya 1996, imefanyiwa marekebisho na sasa Sheria mpya Nam. 7 ya mwaka 2012 inatumika. Sheria hiyo inakwenda sambamba na dhana ya Utalii kwa Wote.

Juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuiimarisha Sekta ya Utalii, zinaendelezwa kwa kasi zaidi na hivi karibuni Sekta ya Utalii imeingizwa katika Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (Results for Prosperity). Mpango huo ulitoa fursa ya kubainisha changamoto mbali mbali zinazoikabili sekta hii na kuzipatia ufumbuzi.

Hivi sasa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza maazimio yaliyopitishwa kwa mujibu wa Mpango wa Matokeo kwa Ustawi (Results for Prosperity). Miongoni mwa maazimio haya ni pamoja na kuendeleza jitihada za kuimarisha vivutio vya utalii kwa kuvilinda vilivyokuwepo na kuengeza vipya, kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato, kuitangaza Zanzibar katika masoko mapya hasa ya Asia ili kuongeza mapato yanayotokana na sekta hiyo.

Juhudi zote hizi zimekuwa ni chachu ya kuvutia watalii na wawekezaji ambao wako tayari kutumia kiwango kikubwa cha rasilimali zao kwa kujenga hoteli za kisasa zinazokidhi mahitaji ya wageni wa aina na daraja zote, kama ilivyoshuhudiwa katika hoteli hiyo. Kufunguliwa kwa hoteli hiyo kunaifanya Zanzibar kuwa na jumla ya hoteli 17 za nyota tano, hoteli 9 za nyota 4, nyengine 43 za nyota 3 na hoteli 6 za nyota 2.

Ni dhahiri kuwa juhudi zinazochukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kushajiisha wawekezaji wa ndani na nje ya Zanzibar kuwekeza katika sekta ya utalii, zimekuwa zinazaa matunda mazuri. Umoja na mshikamano walionao wananchi wa Zanzibar, amani na utulivu iliyopo, mazingira mazuri na historia ya Zanzibar, ukarimu na utamaduni wa watu wa Zanzibar ni baadhi tu ya mambo muhimu yanayoifanya Zanzibar kuwa kivutio cha wawekezaji na wageni kutoka nchi mbali mbali duniani. Mambo hayo ambayo ni adimu katika sehemu nyengine duniani, hayana budi kulindwa na kuenziwa kwa maslahi ya maendeleo ya Zanzibar.

Ni ukweli uliowazi kwamba ukubwa na uzuri wa majengo ya hoteli hiyo ulioshuhudiwa na wapita njia na waliohudhuria kwenye sherehe hizo za ufunguzi, vinatoa sura halisi ya kiwango kikubwa cha fedha zilizotumika katika kuukamililisha





3

1

*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akifuatana na Sheikh Ali Sayeed Albawardy, Mmiliki wa Hoteli ya Park Hyatt Zanzibar alipotembelea sehemu mbali mbali za Hoteli hiyo baada ya kuifungua rasmi tarehe 8 Machi 2015.*

2

*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiagana na Sheikh Ali Sayeed Albawardy baada ya sherehe za ufunguzi wa Hoteli ya Park Hyatt Zanzibar. Katikati ni Meneja Mkuu wa Hoteli hiyo Bi. Mercela Heeendoerfer.*

3

*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe kuashiria ufunguzi wa Hoteli ya Park Hyatt Zanzibar iliyopo Mambo Msiige Mji Mkongwe wa Zanzibar*

mradi huo. Kwa hatua hiyo ni vyema kwa wahusika na hasa watendaji wa Serikali kukumbuka wajibu wao wa kuwapa wawekezaji mashirikiano yanayohitajika na kuondokana na urasimu usiokuwa wa lazima ili kuwapa nguvu, ari na kasi ya kuendesha shughuli zao kwa ufanisi.

Inatia moyo sana kuona kuwa idadi ya hoteli zenye majina na hadhi ya Kimataifa zinaongezeka hapa Zanzibar. Mtandao wa hoteli ya Park Hyatt umejipatia umaarufu mkubwa duniani kote kutokana na ubora wa huduma zinazotolewa. Hivyo kuwepo kwa Hoteli hii kutasaidia sana katika kuitangaza Zanzibar na kutekeleza mikakati ambayo Serikali imejipangia ya kuvutia watalii wa daraja la juu.

Jambo moja linalojidhihirisha kutokana na ujenzi wa hoteli hii ni kubainisha nafasi kubwa iliyopo ya kuufanya Mji Mkongwe uwe mji unaopendeza na kuiongeza hadhi yake pamoja na sifa ya kuwa Mji Mkongwe wenye urithi wa Kimataifa.

Ustadi, ufundi, mtindo na sanaa ya majengo ya zamani vilivyotumiwa na muwekezaji katika kufuata masharti aliyopewa na Serikali ya kujenga majengo ya zamani na kuyageuza kuwa hoteli ya kisasa, vinadhihirisha kuwa mji mkongwe unaweza kuwa mji wenye haiba nzuri zaidi kwa kuwekwa majengo mapya bila ya kuathiri muonekano wake wa kisasa.

Akizungumza kwenye hafla ya ufunguzi wa hoteli hiyo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amewahakikishia wawekezaji wa hoteli hiyo na wawekezaji wengine wote kuwa Serikali itazidi kuimarisha ulinzi katika Mji Mkongwe ili kuhakikisha kuwa sehemu hiyo inayopendwa na watalii inabakia kuwa salama kama zilivyo sehemu nyengine zote za Zanzibar.

Ameiagiza Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuendelea kusimamia kwa karibu shughuli zote za ujenzi, ukarabati na usanifu wa Mji Mkongwe kwa lengo la kuhakikisha kuwa majengo yanayojengwa yanakidhi viwango na hadhi ya kuwa ni sehemu ya Mji Mkongwe kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Serikali na vigezo vya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Aidha, ameliagiza Baraza la Manispaa la Zanzibar kuongeza kasi ya usafi katika wakati huu ambapo limepata vifaa mbali mbali vya kisasa kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao.

Ufunguzi wa hoteli hiyo ni hatua muhimu katika utekelezaji wa "dhana ya utalii kwa wote" ambapo wananchi wataendelea kupata ajira mbali mbali tokea mradi wa ujenzi wa hoteli hii ulipoidhinishwa na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar, tarehe 20 Oktoba, 2010. Wafanyakazi wapatao 150 wameshaajiriwa kwa shughuli za uendeshaji wa hoteli hiyo.

Aidha, kupitia mradi huo, wajasiriamali na wafanyakazi wengi wa sekta binafsi wataweza kunufaika. Ni wazi kwamba hoteli hii itakuwa na manufaa makubwa kwa wajasiriamali wa bustani ya Forodhani, wamiliki wa maduka na mikahawa katika eneo la Mji Mkongwe, wamiliki wa vyombo vya baharini, madereva wa taxi, kampuni za kupokea na kutembeza wageni, wakulima na wavuvi na wananchi wanaojishughulisha na sekta nyengine.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia ramani ya ujenzi wa Barabara za Mkwajuni - Kijini na Matemwe - Muyuni Mkoa wa Kaskazini Unguja inayojengwa na Kampuni ya Pennyroyal Gibraltar Ltd alipotembelea mradi huo tarehe 25 Machi, 2015*

# Ujenzi wa barabara ya Mkwajuni-Kijini na Matemwe-Muyuni umeanza.

Ndoto za muda mrefu za wananchi wa vijiji mbali mbali vya Matemwe kupitia barabara za Kiashange-Kijini-Mbuyutende na Matemwe-Muyuni za kutaka kuona wanapita kwenye barabara ya lami ya kisasa, zimeanza kuyakinika kufuatia kuanza rasmi kwa ujenzi wa barabara hizo zenye urefu wa jumla ya kilomita 17.

Kuanza kwa ujenzi wa barabara hizo, siyo tu kunazidi kufikisha kiwango kizuri zaidi cha utekelezaji wa Ilani ya CCM 2010 – 2015, lakini vile vile kunaondosha minong'ono iliyokuwa imesambaa, kwamba Serikali haitoweza kuanza kuijenga barabara hiyo kama ilivyokuwa imeahidiwa kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2010 - 2015.

Akizungumza na wananchi wa Matemwe wakati alipotembelea ujenzi huo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein aliwaeleza wananchi wa kijiji hicho kuwa ujenzi wa barabara hiyo ni utekelezaji wa ahadi yake aliyoitoa wakati wa kampeni za Uchaguzi mwaka 2010 na kwamba utekelezaji wake umechelewa kidogo kutokana na ukosefu wa nyenzo ikiwemo fedha, vifaa na utaalamu.

Aliwaeleza wananchi hao kuwa ujenzi wa barabara hiyo unafanyika kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza barabara inajengwa kwa kiwango cha kifusi kwa msaada wa kampuni ya Uwekezaji ya Pennyroyal Zanzibar Limited na awamu ya pili itajengwa na Serikali kwa kuitia lami kuanzia mwezi Oktoba mwaka huu baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza.

Alisema kama ilivyo miradi mingine ya aina hiyo kwenye maeneo ya fukwe za bahari, mradi huo unatarajiwa kubadili hali za maisha ya wananchi wa Matemwe Muyuni na kuwa bora zaidi kutokana na kufaidika na huduma mbalimbali ikiwemo ajira, tatizo ambalo limekuwa ndio chanzo cha matatizo mengi miongoni mwa vijana.

Barabara hiyo ya kisasa ya njia mbili inalenga kulifungua eneo hilo kuwezesha uwekezaji wa miradi mikubwa ya kitalii ukiwemo mradi wa "Amber Golf and Beach Resort" utakaoendeshwa na Kampuni ya Pennyroyal.

Mradi huo ambao utajumuisha hoteli na nyumba za kitalii katika pwani hiyo pamoja na kiwanja kidogo cha ndege, unatarajiwa kuwa ni mradi wa aina ya kipekee katika pwani ya Afrika Mashariki.

Ili kufanikisha vyema utekelezaji wa mradi huo, wananchi wametahadharishwa juu ya vitendo vya makusudi vya kujenga katika maeneo ya barabara kwa matarajio



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi na Mmiliki wa Kampuni ya Pennyroyal Bwana Brian Thomson kuhusu ujenzi wa Barabara za Kiashange -Kijini-Mbuyutende na Matemwe-Muyuni katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na miradi mingine ya utalii na kijamii katika eneo la Matemwe - Mbuyuni*

kuwa Serikali itawalipa fidia wakati ujenzi au upanuzi wa barabara hiyo unapofanyika.

Tahadhari hiyo imetolewa baada ya kuonekana harakati za ujenzi wa majengo mapya zinazoendelea pembezoni mwa eneo linalojengwa barabara hiyo ya kisasa. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na wananchi wa Matemwe, alisisitiza kuwa Serikali itavunja majengo yote yaliyomo pembezoni mwa barabara hiyo ili kupisha ujenzi huo lakini fidia ya Serikali itatolewa kwa wale tu ambao nyumba zao zilikuweko tokea awali ambao, alisema wanafahamika.

Aliwataka wananchi kuacha kujenga katika maeneo ya barabara na kuwakumbusha kuwa maeneo yote ya hifadhi ya barabara kuwa yanapaswa kuheshimiwa na kwamba wanaojenga kwenye maeneo hayo wafahamu kuwa watakuwa wanavunja sheria.

Aidha, aliwakumbusha wananchi kuwa ardhi ni mali ya Serikali na pale Serikali inapoamua kuitumia ardhi hiyo kwa manufaa ya taifa wananchi wanaoitumia ardhi hiyo watafidiwa mali zao na kusisitiza kuwa hatua zote hizo zitafanyika kwa kuzingatia sheria zilizopo.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu Dk. Juma Malik Akil barabara za Kiashange – Kijini - Mbuyutende na Matemwe - Muyuni zinaunganisha vijiji vya Kijini, Mbuyutende na Muyuni kutokea barabara kuu ya Mkwajuni-Matemwe.

Dk. Juma alisema barabara ya Kiashange-Kijini-Mbuyutende ina kilomita 9.4 wakati barabara ya Matemwe- Mbuyutende- Muyuni ina kilomita 7.6. Alibainisha kuwa kazi ya michoro na usanifu wa barabara hizo umefanywa na Kampuni ya Intercontinetal Cosultants and Technocrats kutoka India.

Kuanza kwa ujenzi wa barabara hiyo kunaifanya Serikali kufikia kiwango kizuri zaidi katika utekelezaji wa Ilani ya CCM 2010-2015.

Miongoni mwa barabara zinazoendelea kufanyiwa kazi ni pamoja na barabara ya Jendele – Cheju – Kaebona (6.0), Koani – Jumbi (6.4), na Mkwajuni – Kijini (5.5).

Miongoni mwa barabara zilizokamilika ni Mtoni – Amani (4.0), Amani - Dunga (13.2), Pandani – Finya (8.0), Bahanasa – Daya – Mtambwe (13.6), Mzambarau – Karimu mapofu (8.6), Kwale – Kojani (2) na Kipangani – Kangagani (3).

Kazi ya usanifu na utayarishaji wa zabuni umeshakamilika kwa barabara zinazoingia mjini "town entry roads" zenye jumla ya urefu wa kilomita 78, na hatua za kutafuta wafadhili wa kazi ya ujenzi zinaendelea.

Aidha, kazi ya Upembuzi yakinifu "feasibility study" kwa barabara 6 za vijijini Unguja zenye urefu wa jumla kilomita 48, umeshakamilika na usanifu na mchoro wa kiufundi na utayarishaji wa zabuni umeanza.

Vile vile jumla ya barabara 5 zenye urefu wa kilomita 24.3 zipo katika hatua mbali mbali za matayarisho ya ujenzi. Barabara zenyewe ni Mganyageni – Kangani (6.5), Finya – Kicha (8.8), Shumbaviamboni – Tumbe (5) na Kuyuni – Ng'ombeni (4).

# Huduma za afya Zanzibar zazidi kuimarika

## ■ Kampuni ya Vigor imejenga hospitali ya kisasa



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Daktari Mkuu na Mwenyekiti wa Kampuni ya Global Hospital Dk. K. Ravindranath wakati alipotembelea chumba cha wagonjwa mahututi katika Hospitali ya Tasakhtaa iliyopo Mtaa wa Vuga Mjini Unguja baada ya kuifungua rasmi hospitali hiyo tarehe 28 Machi, 2015*

"Mjenga nchi ni mwananchi" ni usemi wa Kiswahili uliodhihirishwa kwa vitendo na kampuni ya Vigor inyoongozwa na mfanyabiashara maarufu Zanzibar Bwana Salim Hassan Turky iliyowekeza hospitali ya kisasa katika eneo la Vuga mjini Unguja.

Uamuzi wa kampuni hiyo wa kujenga hospitali hiyo ya TASAKHTAA hapa Zanzibar kwa kushirikiana na Uongozi wa "Global Hospitals" ya India, ni miongoni mwa matumizi bora ya rasilimali zake kwa lengo la kuimarisha ustawi wa wananchi na uchumi wa Zanzibar.

Ufunguzi wa hospitali hiyo kwa mara nyengine tena unathibitisha kasi ya ukuaji na uimarishaji wa huduma katika sekta ya afya Zanzibar na umefanyika wakati Serikali ikiendelea kukamilisha mipango ya kuifanya hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa Hosptiali ya rufaa ili iweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Katika kufikia azma hiyo, Serikali imeweka vifaa vipya vya kisasa katika chumba cha upasuaji, Wodi ya Wagonjwa Mahtuti na Wodi ya Wazazi.

Vile vile, tarehe 09 Januari, 2015 katika maadhimisho ya miaka 51 ya Mapinduzi ya Zanzibar, kilifunguliwa kitengo cha matibabu ya Ubongo na Uti wa Mgongo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ambacho kimejengwa kwa mashirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Taasisi inayoshughulikia maradhi ya Uti wa Mgongo na Mishipa ya hisia kutoka Hispania (Neurosurgical Education Foundation – NED).

Huduma zinazotolewa na kituo hiki ni adimu kupatikana katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati. Vile vile, katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Serikali imeanza ujenzi wa jengo litakalotoa huduma za watoto na huduma kwa ajili ya maradhi ya figo. Vile vile, Serikali inalifanyia matengenezo makubwa jengo lililokuwa la kiwanda cha dawa kwa kuanzisha wodi ya wazazi, huduma za "clinics" mbali mbali, huduma za wagonjwa wa nje, wagonjwa wanaofikwa na ajali, na kadhalika.

Matengenezo haya yanagharamiwa na Shirika la ORIO la Uholanzi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mbali ya kuimarisha hospitali ya Mnazi Mmoja, hospitali ya Abdalla Mzee iliyopo Pemba inajengwa upya wakati hospitali nyengine nazo zinafanyiwa matengenezo makubwa pamoja na kuzipatia vifaa na nyenzo ili ziweze kutoa huduma bora zaidi.

Kwa upande wa madaktari, Serikali imeongeza kasi ya kusomesha madaktari na wataalamu katika sekta ya Afya. Hivi sasa Serikali imeanzisha mafunzo ya udaktari katika Chuo Kikuu cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA), ambapo jumla ya wanafunzi 82 wapo katika mwaka wa kwanza na wa pili.

Vile vile, takriban wanafunzi 200 wanaosomea mafunzo ya udaktari wapo Tanzania Bara na nje ya nchi. Aidha, mafunzo ya wafanyakazi wa Sekta ya afya katika Chuo cha Taaluma ya Sayansi za Afya, yanakwenda sambamba na mafunzo ya fani ya udaktari katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA). Utekelezaji wa mpango wa kukiunganisha Chuo cha Taaluma ya Sayansi za Afya kuwa ni sehemu ya SUZA unatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Vile vile, mnamo mwezi Septemba mwaka, 2014 kwa mara ya kwanza

Serikali iliwaajiri madaktari 38 waliomaliza mafunzo yao ya udaktari katika Chuo Kikuu cha Mathansas, Cuba, ambao walisomeshwa hapa Zanzibar. Hali hii inatoa mwelekeo wa kulimaliza tatizo la uhaba wa madaktari katika miaka michache ijayo. Hadi mwanzoni mwa mwaka huu daktari mmoja alikuwa akitoa huduma kwa watu 9,708 ikilinganishwa na daktari mmoja kwa watu 18,982 katika mwaka 2014.

Juhudi hizo za kuimarisha huduma na idadi ya wataalamu nchini pamoja na ongezeko la hospitali binafsi za kisasa, kwa pamoja, zitaiwezesha Serikali kwa kiasi kikubwa kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopelekwa nchi za nje kwa ajili ya matibabu. Aidha, juhudi hizo zinaashiria kwamba hivi karibuni Zanzibar itaanza kupokea wageni kutoka nchi mbali mbali kuja kupata matibabu hapa Zanzibar, jambo ambalo kwa muda mrefu lilionekana kama ni ndoto ambayo haipaswi hata kufikiriwa.

Katika kufanikisha utekelezaji wa suala hili kwa ufanisi, Wizara ya Afya haina budi kuendeleza juhudi za kushirikiana na hospitali binafsi na kuhakikisha kuwa sheria ya hospitali binafsi ya mwaka 1994 inatekelezwa ipasavyo na kwamba sheria na taratibu nyengine za afya zinatekelezwa na zahanati na hospitali za watu binafsi.

Akifungua hospitali hiyo ya TASAKHTAA, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amewahakikishia wananchi kuwa jitihada za Serikali za kuhamasisha uwekezaji na kushiriki kwa sekta binafsi katika sekta ya afya hazina dhamira ya kubadilisha malengo ya Waasisi wa Mapinduzi ambayo yalitilia mkazo usawa na haki ya kila mtu kufaidika na huduma za Afya zinazotolewa na Serikali.

Alisema juhudi za Serikali za kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya afya zina lengo la kukidhi na kwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yanayotokea ndani na nje ya nchi. Kuwepo kwa hospitali za Serikali na binafsi kwa pamoja kunatoa fursa pana zaidi kwa wananchi kuchagua sehemu za kufuata huduma kwa mujibu wa mahitaji, urahisi na uwezo walionao. Alisisitiza kuwa Sera ya Msingi ya Huduma za Afya, ya Serikali kutoa matibabu bila ya malipo ipo pale pale.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na wananchi, viongozi na wawekezaji mbali mbali waliohudhuria sherehe za ufunguzi wa Hospitali ya Tasakhtaa*

"napenda ifahamike kwamba Serikali ilifanya uamuzi wa kuwataka wananchi wachangie huduma za afya kutokana na hali ya uchumi iliyoikabili Serikali katika miaka ya 2000. Hata hivyo, utaratibu wa kuchangia bado haujaandaliwa vizuri na kazi hiyo hivi karibuni inakamilishwa na itatangazwa rasmi hapo baadae". Alisema Dk. Shein.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa pongezi maalum kwa Mheshimiwa Turky kwa uamuzi wake wa kutumia sehemu ya rasilimali yake kuinua ustawi wa maisha ya wananchi wa Zanzibar kwa kuwekeza katika miradi tofauti.

Miradi mingine ya Mheshimiwa Turky ambayo imesaidia kutoa ajira kwa wananchi kadhaa wa Zanzibar ni pamoja na Hoteli ya "Grand Palace", kiwanda cha kutengenezea vinywaji mbali mbali – "Zainab Bottlers Ltd" na kampuni inayoshughulikia uingizaji na usafirishaji wa bidhaa – "Zenj General Merchandise Ltd".



*Mwenyekiti wa Kampuni ya Vigor Turky ambaye vile vile ni Mbunge wa Mpendae Mhe. Salim Hassan Turky akitoa salamu zake kwenye sherehe za uzinduzi wa Hospitali ya Tasakhtaa iliyopo Mtaa wa Vuga Mjini Unguja tarehe 28 Machi, 2015*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame akimkabidhi zawadi ya mlango mmoja wa washiriki wa michezo ya Pasaka kutoka Dar es Salaam katika sherehe zilizofanyika kwenye hoteli ya Zanzibar Ocean View ya Chuini tarehe 04 Aprili 2015*

# Dk Shein: Ziara za Michezo ya Pasaka zinaimarisha udugu, urafiki na Muungano wetu

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amezipongeza klabu za michezo za Ikulu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa kuendeleza ziara za michezo ya Pasaka ambazo alielezea kuwa lengo lake ni kuimarisha udugu, urafiki na muungano kati ya wananchi wa Zanzibar na Tanzania Bara.

Katika pongezi zake hizo zilizotolewa kwa niaba yake na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora Mheshimiwa Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini wakati wa chakula cha usiku kwa ajili ya kuwaaga wanamichezo wa timu ya Ikulu ya SMT, Dk. Shein alisema michezo ya Pasaka ni "kielelezo cha umoja wetu, urafiki wetu na muungano wetu".

Katika salamu hizo alisema yeye na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Jakaya Mrisho Kikwete wanafuatilitia kwa karibu michezo hiyo ambayo ina historia ya pekee katika kujenga na kuimarisha mahusiano kati ya watu wa Zanzibar na Tanzania Bara.

Kwa hivyo walieleza kuwa viongozi wa timu hizo hawana budi kuhakikisha kuwa michezo hiyo inaendelezwa kwa kuendelea kutembeleana kila mwaka.

Mwaka huu timu ya Ikulu ya Zanzibar imekuwa mwenyeji wa Ikulu ya SMT ambapo katika mashindano ya michezo mbalimbali iliyochezwa kati ya timu hizo, timu ya Ikulu SMT ilichukua ushindi wa jumla.

Akizungumza katika halfa hiyo kumkaribisha mgeni rasmi, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ndg. Said Natepe, aliwapongeza viongozi wa klabu zote mbili kwa kufanikisha michezo katika ziara hiyo ya siku tatu.

Naibu Katibu Mkuu huyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Klabu ya Michezo ya Ikulu Zanzibar alieleza kufurahishwa kwake na jinsi wanamichezo wa klabu hizo wanavyoonesha upendo, mshikamano na urafiki miongoni mwao.

Katika hafla hiyo Waziri Mwinyihaji alimkabidhi kombe la ushindi wa jumla nahodha wa Klabu ya Ikulu SMT Nd. Hassan Ekoni na pia alimkabidhi Katibu wa Timu hiyo Ndg. Ramadhani Bendera zawadi maalum ya Mlango wa Asili wa Zanzibar kama kumbukumbu ya ziara yao.

Katika maelezo yake mafupi Katibu wa Timu ya Ikulu SMT Ndg. Ramadhani Bendera aliishukuru Ikulu ya Zanzibar kwa kuonesha urafiki na udugu wa kweli wakati wote wanamichezo wa klabu yake walipokuwa ziarani Zanzibar.

Bwana Bendera aliwahakikishia wenyeji wake kuwa klabu yake imejiandaa vyema kuwapokea mwakani wakati wa ziara yao huko Tanzania Bara.

# Dk. Shein atembelea maendeleo ya ujenzi wa uwanja wa ndege Zanzibar



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa Msimamizi wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Abiria "Terminal II" katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Bwana Yasser De Costa wakati alipofanya ziara maalum ya kuangalia maendeleo ya ujenzi wa mradi huo tarehe 9 Aprili, 2015*

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imeshapiga hatua kubwa katika kutekeleza majukumu yake na kufikia malengo yaliyowekwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2010 – 2015.

Imeelezwa kwenye Ilani hiyo ambayo inakwenda sambamba na MKUZA II, Dira ya 2020 na malengo Milenia kwamba, usafiri wa anga ni moja kati ya nyenzo muhimu za kukuza uchumi, na ni kichocheo cha kuendeleza sekta ya utalii. Ili kuiendeleza zaidi sekta ya usafiri wa anga, katika kipindi cha miaka mitano (2010-2015), Serikali imekusudia kutekeleza kazi mbali mbali ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa mpango mkuu wa uendelezaji wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Zanzibar na kusimamia ujenzi wa jingo jipya la abiria.

Aidha, Serikali ilipanga kukamilisha kazi za ujenzi wa uzio, kuweka taa katika bara bara za kurukia na kutulia ndege pamoja na kuimarisha huduma za umeme kwa kukipatia generator la akiba kiwanja cha ndege cha Karume Pemba.

Suala jengine muhimu lilikuwa ni kuwapatia mafunzo na vifaa vya kisasa wafanyakazi wa Viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba sambamba na kuimarisha huduma za zimamoto na usalama wa jumla kwenye viwanja vya ndege.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein hivi karibuni alitembelea uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume kuona maendeleo ya utekelezaji wa kazi mbali mbali zilizopangwa kutekelezwa kwa mujibu wa mpango wa kitaifa MKUZA II na Ilani ya CCM 2010-2015.

Sheria nambari 8 ya 2011 ya kuanzishwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilipitishwa rasmi na Serikali baada ya kuingia madarakani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Pamoja na mambo mengine sheria hiyo inaipa uwezo wa kisheria Mamlaka kuviendesha, kuvisimamia, na kuvitunza viwanja vya ndege vya Serikali katika Zanzibar, kutoa huduma za kuridhisha za ufanisi na za kiusalama kwa safari za abiria na mizigo katika viwanja vya ndege vya Serikali.

Mamlaka vile vile imepewa uwezo wa kisheria kuhakikisha kwamba sera za viwanja vya ndege vya Zanzibar, kanuni na taratibu zinatekelezwa kwa mujibu wa viwango na taratibu za kimataifa zilizopendekezwa: pamoja na sheria za Zanzibar na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazotumika Zanzibar.

Vile vile Mamlaka ina jukumu la kuweka miundombinu muhimu, vifaa na huduma katika viwanja vya ndege, kuhakikisha usalama, kusimamia viwango vya usalama

ndani ya uwanja wa ndege na maeneo ya karibu na uwanja wa ndege pamoja na kusimamia ardhi iliyo katika mipaka ya uwanja wa ndege.

Katika uendeshaji na utekelezaji wa majukumu yake Mamlaka imejikita zaidi katika kujenga uwezo wa wafanyakazi, kuboresha mazingira ya kazi kwa kufuata sheria na taratibu pamoja na kuboresha ulinzi na usalama katika maeneo yote ya viwanja vya ndege.

Mamlaka ina jumla ya wafanyakazi 385 wa kudumu kwa Unguja na Pemba kati yao Unguja ni 314 na Pemba ni 71. Lakini ili kuongeza uwezo wa kiutendaji na ufanisi, Mamlaka imechukua juhudi maalum kuwajenga uwezo wafanyakazi wake.

Katika kipindi cha miaka minne iliyopita Mamlaka imeweza kuwapatia mafunzo ya muda mrefu ngazi ya Cheti, Diploma, Degree ya kwanza na ya pili katika fani mbali mbali jumla ya wafanyakazi 70.

Aidha, jumla ya wafanyakazi 251 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya masuala mbali mbali yanayohusiana na usalama, urushaji na uegeshaji wa ndege ndani na nje ya nchi. Sambamba na juhudi hizo, wafanyakazi 23 wenye elimu ya juu katika fani tofauti wamehamishiwa kutoka taasisi mbali mbali za Serikali kwa ajili ya kuimarisha nguvukazi kwenye Mamlaka hiyo.

Miongoni mwa wafanyakazi hao wamepatiwa mafunzo kuhusiana na namna ya Mamlaka kuweza kuviendesha viwanja vyake kulingana na sheria na taratibu za Kitaifa na Kimataifa. Ili kuendana na viwango hivyo, Mamlaka imekuwa ikilazimika kuweka mazingira ya kazi yanayozingatia ufuataji wa sheria na taratibu zilizowekwa na kuwataka watumiaji wa viwanja, kufuata sheria, miongozo na maelekezo kama yanavyotolewa na maafisa husika.

Kuhusu suala la ulinzi na usalama, Mamlaka imeshachukua hatua kadhaa ili kuhakikisha kuwa suala la ulinzi linaimarika katika kiwango kinachokubalika Kitaifa na Kimataifa.

Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kununua mashine nne mpya za kukagulia mizigo ya abiria, kuboresha mfumo wa ulinzi kwa kutumia kamera mpya za kisasa na kusaidia kuimarisha huduma za zimamoto kwa kununua vipuri na kutoa mafuta ya kuendeshea magari ya zimamoto.

Hatua nyengine muhimu zilizochukuliwa na Mamlaka katika kuimarisha ulinzi na usalama ni pamoja na kuimarisha mfumo wa ulinzi kwa kutumia kamera maalum "Closed Circuit Television"- CCTV" kwa kuzibadilisha baadhi ya kongwe na kuweka mpya .

Mamlaka kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeanza ujenzi wa ukuta wa uzio unaolizunguuka eneo lote la Uwanja wa "Abeid Amani Karume International Airport(AAKIA). Katika hatua ya sasa lipo eneo ambalo limeshakamilika na eneo jengine ujenzi unaendelea.

Aidha, Mamlaka imekodi kikosi cha Valantia (KVZ) kwa ajili ya kulinda usalama katika maeneo ambayo ukuta bado haujajengwa na maeneo ambayo kuna uwezekano wa kufanyika uharibifu wa mazingira ili kuepusha athari zaidi.

Vile vile mamlaka imefanikiwa kuwatenganisha abiria wanaosafiri ndani ya nchi "domestic flights" na wale wanaosafiri nje ya nchi "international flights" kwa kujenga ukumbi mpya unaotumiwa na abiria wa ndani. Hatua hiyo imesaidia kuondoa usumbufu wa muda mrefu wa msongomano wa abiria uliokuwa ukitokea wakati wa kusafiri.

Katika jitihada zake za kuleta maendeleo katika viwanja vyake, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, imeanzisha miradi mbali mbali kwa lengo la kuboresha huduma na kuongeza mapato ya Mamlaka. Hadi sasa kuna jumla ya miradi minne (4) ambayo Mamlaka imeianzisha kwa madhumuni hayo.

Mradi wa maegesho ya magari unalenga kuboresha huduma uwanjani, kudhibiti uingiaji na utokaji wa magari katika eneo la maegesho. Mradi huu unasaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa kiwanja cha ndege pamoja na kuiongezea mapato Mamlaka.

Vile vile Mamlaka imefanya ujenzi wa kumbi mbili za kuwahudumua abiria wa daraja la kwanza kwa abiria wanaoondoka na abiria wanaowasili. Aidha, Mamlaka imekusudia kufanya wa eneo la ukumbi wa abiria wanaoondoka pamoja na kuboresha huduma zote muhimu katika ukumbi huo. Sambamba na hilo, ukumbi wa abiria wanaowasili nao vile vile utafanyiwa utanuzi kwa lengo la kutoa nafasi zaidi kwa abiria.

Mamlaka imeanzisha mradi wa eneo la kituo cha biashara kwa ajili ya kupanua huduma uwanjani. Eneo hilo linatoa huduma mbali mbali zikiwemo huduma za kiofisi, huduma za kibenki na huduma za vyakula na vinywaji.

Kadhalika, Mamlaka inatarajia kuanza mradi wa ujenzi wa taa za uwanjani katika Uwanja wa Ndege wa Pemba ambapo hatua za awali za utekelezaji wa mradi huo tayari zimeshaanza.

Mamlaka ya Uwanja wa Ndege Zanzibar kama zilivyo taasisi nyengine, nayo katika mchakato wake wa maeneleo imekuwa ikikabiliana na changamoto mbali mbali ambazo imekuwa ikikabiliana nazo kwa kushirikiana na Serikali kuu.

Hivi sasa Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali kuu inaendelea kuifanyia kazi changamoto ya wafanyakazi wanaohitajika mara baada ya kukamilika mradi wa jengo jipya "New Terminal Building" pamoja na kufanya tathmini ya gharama zitakazohitajika katika kuliendesha jengo hilo la kisasa.

Vile vile Mamlaka inaendelea na kufanya tathmini ya gharama za uendeshaji zitakazoongezeka mara baada ya kukamilika kwa ujenzi huo ambapo licha ya kulazimika kulipa mkopo wa fedha zilizotumika kwa ununuzi wa mashine za kukagulia mizigo, italazimika vile vile kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kugharamia ulinzi kwa kikosi cha KVZ kwenye maeneo ambayo hayana kamera maalum. Kiasi ya Tsh milioni 20 hulipwa kila mwezi kwa ajili ya matumizi hayo.

Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji ya Mamlaka hiyo, mapato halisi yanayokusanywa na Mamlaka hiyo kwa sasa hayawezi kukidhi matumizi ya lazima ya uendeshaji wa viwanja vya ndege. Wastani wa makusanyo wa mapato kwa mwezi ni Tzs milioni 300, wakati wastani wa matumizi ya lazima kwa mwezi ni Tzs 375.5.




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikabidhiwa Jezi nambari 14 ya timu ya Barcelona FC na mchezaji wa zamani wa timu hiyo na kocha Johan Cruyff wakati wa chakula kilichoandaliwa maalum na Rais wa Zanzibar kwa wachezaji wa zamani wa klabu hiyo Ikulu Zanzibar tarehe 9 Aprili 2015*

# Magwiji wa zamani wa Barcelona wakaribishwa Ikulu

## ■ Ni jitihada za SMZ kutaka kuinua soka

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) iliwaalika Ikulu mjini Zanzibar wachezaji wa zamani wa mchezo wa mpira wa miguu ya Barcelona ya Hispania ikiwa ni miongoni mwa jitihada za kutaka kuimarisha mchezo huo hapa Zanzibar.

Ni ukweli uliowazi kwamba Zanzibar imejijengea umaarufu wa siku nyingi katika mchezo huo na jitihada mbali mbali zimekuwa zikichukuliwa na Serikali ili kuhakikisha kuwa hadhi ya mchezo huo na aina nyengine za michezo inakuwa endelevu.

Miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na kuonesha wazi kibajeti umuhimu wa michezo katika mipango ya maendeleo ikizingatiwa kwamba, zama hizi zimeufanya utamaduni na michezo kuwa sehemu ya diplomasia ya uchumi kwa nchi inayohusika.

Jitihada nyengine za kuendeleza michezo ni kuweka mkakati endelevu wa kuinua na kuendeleza michezo ya riadha sambamba na kuandaa mkakati wa kuwatambua vijana wenye vipaji mbali mbali vya michezo na kuwaendeleza.

Akizungumza na wachezaji hao wa zamani wa timu ya Barcelona, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alisema pamoja na Zanzibar kuwa na vijana wengi wenye vipaji katika mchezo wa soka lakini kukosekana kwa

☛ Uk.18

# Matukio katika Picha



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akizungumza na Balozi wa Jamhuri ya Uholanzi nchini Tanzania Bwana Jaap Fredriks alipofika Ikulu Mjini Zanzibar tarehe 2 Machi 2015*




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na viongozi mbali mbali alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Songea Mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya uzinduzi wa mbio za mwenge wa Uhuru Kitaifa katika uwanja wa Majimaji Songea Mkoani humo uliofanyika tarehe 29 Aprili, 2015*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ikiwa ni ishara ya kulifungua Jengo jipya la Afisi Kuu ya Uhamiaji Zanzibar liliopo Kilimani Mjini Unguja tarehe 25 Aprili, 2015. Kulia ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Pereira A. Silima akifuatiwa na Kamishna wa Uhamiaji Sylvester Ambo Kile*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na viongozi wa Baraza la Michezo la Taifa wakiwa katika picha ya pamoja na wachezaji wa zamani wa timu ya soka ya Barcelona ya Hispania walipotembelea Ikulu Zanzibar tarehe 9 Aprili, 2015*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akipata maelezo kutoka kwa mshauri mwelekezi wa Kampuni ya Adpi ya Ufaransa Bwana Guillaume Verna katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume wakati alipofanya ziara maalum ya kuangalia maendeleo ya ujenzi wa mradi huo tarehe 9 Aprili, 2015*



*Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mama Mwanamwema Shein, akiangalia bidhaa zinazozalishwa na Wanawake Wajasiriamali wa Kikundi cha Sanaa cha Maigizo wakati wa maonesho ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani yalioandaliwa na Kikundi cha "Zanzibalicious Women Group" yaliofanyika viwanja vya hoteli ya Bwawani Zanzibar tarehe 21 Aprili, 2015*

mawakala wenye sifa katika mchezo huo ni mojawapo ya sababu zinazowakosesha vijana hao fursa ya kucheza mchezo huo katika ngazi ya kimataifa.

Dk. Shein aliwaeleza wachezaji hao kuwa Zanzibar ingependa kuwa na uhusiano wa karibu na mawakala mashuhuri wa mpira wa miguu duniani ili kutoa fursa kwa vijana wa Zanzibar kushiriki mchezo huo katika ngazi ya kimataifa kama ilivyo kwa vijana wa nchi nyingine.

Mazingira halisi ya mchezo wa mpira wa miguu yamebadilika kabisa katika miaka ya hivi karibuni kutoka kuwa sehemu ya burudani na kujenga afya miongoni mwa wachezaji na washabiki, na kuwa sehemu ya ajira kubwa miongoni mwa wachezaji, na biashara kwa mawakala wa mchezo huo.

Dk. Shein alisema kuwa ni jambo la kufurahisha kuona jamii hivi sasa inaitumia michezo kuwa sehemu ya kutoa ajira huku ikiwa ni chombo cha kuhimiza upendo, amani, utulivu na kuunganisha watu wa mataifa mbalimbali duniani. "Tunafurahi sana kuona timu ya Barcelona iko msatari wa mbele katika kufanya hivyo, nasi tunawatakia mafanikio mema zaidi" aliongeza.

Kwa upande wa Zanzibar Serikali imevifanyia matengenezo makubwa viwanja vya michezo vya unguja na pemba sambamba na kuimarisha chuo cha mchezo wa mpira wa miguu ambacho kitaibua vipaji vya vijana katika soka.

"Serikali inatilia mkazo mchezo huu na tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali kuuendeleza ili kwenda sambamba na mabadiliko yanayotokea na kukidhi mahitaji ya kisasa ya mchezo huo ikiwemo kuanzisha skuli maalum kwa wototo wenye vipaji, ingawa hazilingani na ile ya Barcelona maarufu -La Masia ambayo ni kitovu cha kutoa wachezaji wenye vipaji" alisema Dk. Shein.

Uamuzi wa kuwaalika wachezaji hao Ikulu unaonesha dhamira ya kweli ya Serikali ya kuweka umuhimu wa michezo katika mipango yake ya maendeleo kwa kuzingatia kwamba, mchezo wa soka na aina nyengine za michezo hazibakii kuwa sehemu ya burudani na kujenga afya pekee, lakini vile vile ni sehemu muhimu ya utalii ambao umekuwa ukichangia sehemu kubwa ya pato la taifa katika uchumi wa Zanzibar.

"mchezo wa mpira wa miguu ni mashuhuri hapa Zanzibar kama ilivyo katika sehemu nyingine duniani, hivyo ujio wenu utawapa fursa wanasoka wa Zanzibar na washabiki wa timu ya Barcelona kuonana uso kwa uso na kujifunza kutoka kwenu mbinu za mchezo huo". Aliongeza Dk. Shein katika mazungumzo yake na wanamichezo hao.

Wachezaji wa zamani na viongozi wa timu hiyo walifika Ikulu kumtembelea Mheshimiwa Rais na kuungana na viongozi wengine wa Serikali, vyama vya michezo pamoja na wanasoka wa zamani wa Zanzibar kupata chakula cha mchana.

Katika hotuba hiyo fupi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliwaomba wachezaji na viongozi wa timu hiyo kuwa mabalozi wa Zanzibar katika kutangaza vivutio vya utalii vya humu nchini kwani michezo na utalii hivi sasa ni vitu vinavyokwenda kwa pamoja.

"Zanzibar imejaaliwa na vivutio vingi vikiwemo sehemu za kihistoria, fukwe nzuri, mandhari maridhawa, ukarimu na urafiki wa watu wake na michezo mingi ya baharini, hivyo nina furaha kuwakabidhi kazi ya kutangaza utalii Zanzibar huko kwenu" Dk. Shein aliwaambia wachezaji hao.

Dk. Shein alitoa shukrani maalum kwa Bwana Rayco Garcia ambaye ni mratibu wa kusaka vipaji wa timu ya Barcelona anayeshirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Tanzania-NSSF kwa kuipokea vyema rai yake ya kutaka timu hiyo izuru Zanzibar wakati walipokutana mjini Dar es Salaam Disemba mwaka jana. Aidha alizipongeza kampuni za Prime Time Promotion na Tanzania Legends Cup kwa kufanikisha ziara ya timu hiyo humu nchini.

Akizungumza katika hafla hiyo Rais wa Heshima wa Timu ya Bacelona Johan Cruyff, alisema ziara yao nchini imelenga kuwatia hamasa vijana na kujifunza kutoka wachezaji hao maarifa katika mchezo wa soka na hata maisha yao ya kila siku.

"Ziara hii itatupa fursa kuonesha maarifa yetu katika mchezo wa soka na pia kuwaelimisha vijana na wananchi kwa jumla kile ambacho sisi tumekuwa tukifanya katika maisha yetu" alieleza Johan Cryuff ambaye pia ni mchezaji wa zamani wa timu ya Taifa ya Uholanzi.

Wachezaji hao mashuhuri ni watu ambao wana sifa ambazo jamii inaweza kujifunza na kujenga kujiamini na kujitambua mambo ambayo ni muhimu katika kufanikisha maisha ya mwanadamu na hasa vijana.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Zanzibar-BMZ Ndg. Khamis Abdalla Seif alieleza kuwa mwaliko wa Mhe. Rais kwa wageni hao ni kielelezo cha muendelezo wa jitihada zake binafsi na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuendeleza michezo nchini.

"Tunakushukuru sana kwa kukubali kukutana na timu hii kitendo ambacho kinatoa ujumbe kwa vijana wetu kuwa Serikali inathamini michezo na hivyo kuwatia ari na hamasa kushiriki" alieleza Makamu Mwenyekiti huyo wa BMZ.

Alieleza ziara hiyo kuwa ni muhimu siyo tu katika kuimarisha mchezo wa mpira wa

miguu Zanzibar, lakini vile vile ni muhimu sana katika kuinua biashara ya utalii Zanzibar.

Ikiwa hapa Zanzibar timu hiyo ilitembelea sehemu mbalimbali za historia na kufanya maonesho ya mpira kwa vijana na wachezaji wa zamani katika uwanja wa Amaan.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akimkabidhi Kikombe Mwenyekiti wa Jimbo la Uzini CCM Ali Shaaban wakati wa sherehe ya kukabidhi vifaa vya Michezo kwa timu 40 za Jimbo la Uzini vilivyotolewa na Mwakilishi wa Jimbo hilo Mohamed Raza katika uwanja wa Mpira Bambi tarehe 12 Aprili, 2015*

# Uzini watakiwa kuwakusanya wanamichezo mahiri

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ametoa wito kwa wanamichezo wa Jimbo la Uzini katika Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini – Unguja, kuanza kufikiria namna ya kuibua vipaji vya wanamichezo na hatimaye kuwakusanya wanamichezo mahiri katika jimbo lao ili kuwa na timu moja ambayo itawajumuisha wachezaji mahiri kutoka kila timu, kama vile inavyofanywa kwa timu za Taifa.

Hatua hiyo itakuwa inakwenda sambamba na malengo ya muda mrefu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha hali ya michezo Zanzibar ambayo yaliwekwa miaka michache baada ya Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari 1964.

Kwa kutambua umuhimu wa michezo, mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya 1964, Serikali ilichukuwa hatua madhubuti za kuendeleza michezo mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuunda Baraza la Michezo, ambalo pamoja na mambo mengine, lililenga kulijenga jina, sifa, hadhi na heshima ya Zanzibar ndani na nje ya mipaka ya Zanzibar.

Malengo mengine makuu ya Baraza hilo yalikuwa ni kutekeleza kwa ukamilifu, kunyanyua na kuendeleza kwa moyo wa kimapinduzi azma ya ASP katika kuleta uelewano baina ya vijana mbali mbali Zanzibar, Tanzania Bara, Afrika na Ulimwenguni kote. Kutokana na ukweli kwamba vijana ndio nguvu kazi inayofaa katika sekta nyingi za maendeleo, mwaka 1968 Baraza hilo liliwekwa chini ya Umoja wa Vijana wa ASP.

Baraza liliweka umuhimu mkubwa juu ya haja ya kuimarisha michezo yote iliyokuwa ikipendwa na kuchezwa na wananchi wa Zanzibar. Miongoni mwa Michezo hiyo ni Mpira wa Miguu, Riadha, Mpira wa magongo, Mpira wa Mezani, Mpira wa Sakafuni (Tennis) na Mpira wa Mikono.

Aina nyengine ya michezo ilikuwa ni Mpira wa Kikapu, Voliboli, Mpira wa Vinyoya, Mchezo wa kuogelea, Bao, karata na michezo mengine ya asili. Baada ya Mapinduzi, Serikali iliajiri baadhi ya makocha na wakufunzi kutoka nje ya nchi kuja Zanzibar kufundisha michezo hiyo.

Ili kuweza kuyafikia melengo hayo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein imeamua kuyafufua na kuyapa nguvu mashindano ya michezo ya aina mbali mbali kuanzia ngazi za chini, jambo ambalo litawezesha kujenga misingi imara ya kimichezo katika ngazi za juu.

Akizungumza na wanamichezo mbali mbali wa jimbo la Uzini ambao walihudhuria sherehe maalum ya kukabidhiwa vifaa vya Michezo vilivyotolewa na Muwakilishi wa Jimbo hilo Mheshimiwa Mohamed

Raza, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alisema hafla hiyo ni mfano mzuri unaoonesha nguvu na umuhimu wa michezo katika kuunganisha, na kujenga jamii yenye vijana wenye nguvu, uzalendo kwa nchi yao na upendo baina yao.

Aliwataka wanamichezo hao kufahamu kwamba nguvu zilizowaunganisha watu kupitia hafla kama hizo, ndizo zilizotumika katika kuwaunganisha wazee wa Zanzibar hadi wakaweza kuunda jumuiya na baadae Chama cha siasa kilicholeta ukombozi wa Zanzibar. Hiyo ni historia ndefu ambayo vile vile inaelezea harakati za wanyonge katika kujipatia ukombozi.

"Alieyekuwa haijui historia hii nakupeni kazi ya nyumbani, ya kwenda kuisoma historia ya nchi yenu na historia ya ukombozi wa wanyonge". Alisema Dk. Shein.

Kwa upande wa viwanja vya michezo, tarehe 17 Septemba 1967, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume aliwakusanya vijana na wananchi wengine kwa ajili ya kuanza kufyeka eneo la Sebleni ili kupata eneo la kujenga Kiwanja cha Amaan. Vijana na Wananchi walihamasika kufanyakazi kwa kujitolea na ilipokifa tarehe 26 Machi, 1968 jiwe la Msingi kwa ajili ya Ujenzi wa Kiwanja hicho liliwekwa na Marehemu Baba wa Taifa, Mawalimu Julius Nyerere.

Ujenzi wa uwanja huo ulikwenda kwa kasi kubwa kutokana na ari ya wananchi kujitolea, hali ambayo ilifanikisha kufunguliwa rasmi uwanja wa Amaani tarehe 12 Januari 1970. Kiwanja hiki kilitoa mchango mkubwa katika kuendeleza mpira wa miguu, riadha na michezo mengine.

Juhudi hizo pamoja na hatua nyengine zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ziliiwezesha Zanzibar kushiriki katika michezo mbali mbali katika ngazi za Kimataifa na kuweza kufanya vizuri katika michezo mingi iliyokuwa ikishiriki.

Vile vile, wachezaji wa Zanzibar walipata sifa nyingi kwa ile michezo ambayo wachezaji wa Zanzibar walikuwa wakishirikiana na wenzao wa Tanzania Bara kwa ajili ya kuiwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mashindano mengine ya Kimataifa.

Ni ukweli uliowazi kwamba katika kipindi cha takriban miaka 15 iliyopita, sifa hiyo ya michezo ndani na nje ya Zanzibar ilianza kupungua. Lakini jitihada binafsi zinazochukuliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ikiwemo kukutana na baadhi ya wanamichezo maarufu wa zamani Zanzibar, kuwaalika wanamichezo mashuhuri kutoka nchini Hispania na kudhamini mashindano mbali mbali, zimekuwa zikitia matumaini makubwa ya kurejesha hadhi ya michezo hapa Zanzibar.

Umuhimu wa michezo kwa maendeleo ya Zanzibar na Tanzania kwa jumla upo wazi na umetiliwa mkazo katika Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA) na Ilani ya CCM ya 2010-2015 iliyotayarishwa kwa ajili ya Uchanguzi Mkuu wa mwaka 2010.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na mtoto mwanamichezo Munira Khamis wa Bambi baada ya kumalizika kwa sherehe za utoaji wa vifaa vya michezo kwa Jimbo la Uzini tarehe 12 Aprili, 2015*

Moja kati ya ishara zinazothibitisha kuongezeka kwa ari ya michezo Zanzibar ni pamoja na kuongezeka kwa vikundi vya mazoezi ya viungo katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba ambavyo vimekuwa vikitembeleana. Hili ni jambo la kufurahisha ikitiliwa maanani kwamba ushiriki huo siyo tu unasaidia katika kuhuwisha afya za wanamichezo na kupambana na maradhi mbali mbali, lakini vile vile unasaidia katika kujenga udugu na mashirikiano miongoni mwa makundi yanayoshiriki.

Kutokana na kutambua na kuthamini vikundi hivyo, Serikali imeanzisha na imekuwa ikiadhimisha Bonanza Maalum la Mazoezi ya Viungo linalofanyika kila ifikapo tarehe 1 Januari ya kila mwaka ambalo hutoa fursa ya kuvikutanisha vikundi vikubwa vyote vya Mazoezi vya Unguja na Pemba.

Ili kuhakikisha kuwa juhudi hizo za Serikali zinakuwa endelevu, SMZ imeandaa mpango maalum wa kutafuta na baadae kuviendeleza vipaji mbali mbali vya michezo viliopo nchini. Tarehe 9 Aprili, 2014 Serikali ilipokea wachezaji mashuhuri waliokuwa wakiichezea Timu ya Barcelona na viongozi wao (Barcelona Veteran) kufuatia mualiko waliopewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein mwezi wa Disemba 2014.

Katika mazungumzo yake na ujumbe huo, Dk. Shein alizungumzia juu ya kuwepo uwezekano wa ujumbe huo kuisaidia Zanzibar kuendeleza vipaji vya vijana wake na uwezekano wa kusaidia kupata mapromota wazuri kwa wachezaji watakaobainika kuwa na vipaji tokea wadogo katika timu za Unguja na Pemba.

Aidha, Serikali kupitia wachezaji hao inaangalia uwezekano wa kusaidiwa kupatiwa mafunzo ya mpira wa miguu kupitia vituo maalum vya michezo (Sports Academies) ambavyo tayari vimeshaanzishwa, ingawa viko katika hatua za awali.

# ZSSF yaanzisha mafao mapya

## ■ Imezindua mfumo mpya wa kuchangia kwa hiari na mafao ya uzazi



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk.Ali Mohamed Shein akimkabidhi cheti cha shukrani Bi Fatma Mohamed Abass akiwa mtumishi wa Awali wa ZVSSS baada ya kuufungua mkutano wa kwanza wa siku mbili wa Wadau wa ZSSF wa siku mbili katika ukumbi wa Salama Hoteli ya Bwawani Mjini Unguja tarehe 21 Aprili, 2015. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya ZSSF Dkt. Suleiman Rashid*

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Zanzibar Social Security Fund – ZSSF) umezidi kuimarika baada ya kuanzisha huduma nyengine zitakazowahusisha moja kwa moja na kwa aina ya kipekee kinamama wanaojifungua na watu wanaojiajiri wenyewe.

Uamuzi huo utaondoa dhana potofu ambayo imejengeka miongoni mwa baadhi ya watu kwamba, mfuko huo ni maalum kwa ajili ya watu walioajiriwa na kwamba unawaweka pembeni wananchi waliojiajiri wenyewe na wale walio nje ya ajira rasmi.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ambaye alikuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa mkutano wa wadau wa ZSSF katika ukumbi wa Salama – hoteli ya Bwawani Zanzibar hivi karibuni, alisema uamuzi wa taasisi hiyo wa kutoa fao la uzazi kwa kinamama wanaojifungua na kuanzisha mchango wa hiari kwa wanachama wanaojiajiri wenyewe ni ishara ya kuwa uwezo wa ZSSF unazidi kuimarika.

Hatua hiyo ni muhimu katika kufikia malengo ya muda mrefu ya ZSSF ambayo imedhamiria vile vile kutoa mafao mengine muhimu kama ya ulemavu, urithi na matibabu. Ipo kila ishara kwamba taasisi hii itaweza kufikia malengo hayo muhimu iliyojiwekea ya kuwanufaisha wateja wake na wananchi kwa kuwapatia mafao mbali mbali katika siku au miaka michache ijayo.

Mfumo mpya wa kujichangia katika mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa hiari ni utaratibu mzuri ambao bila ya shaka utakuwa ni hatua muhimu ya kuwanufaisha wafanyakazi hasa wale walio katika sekta zisizo rasmi. Utaratibu huu ambao ulianzishwa katika kipindi cha majaribio umeonekana kuwa utaweza kuleta tija kubwa hasa katika kipindi hiki, ambacho Serikali imekuwa ikishajiisha jamii kufanya kazi kwa kujiajiri badala ya kutegemea ajira kutoka Serikalini.

Kadhalika utaratibu huu hapa Zanzibar utakuwa na umuhimu wa kipekee hasa ikitiliwa maanani kwamba wananchi wengi bado wanadhani kwamba ZSSF ipo kwa wafanyakazi wa Serikali na wenye kufanya kazi katika kampuni na mashirika makubwa tu.

Utaratibu wa kuwa na Hifadhi

ya Jamii una historia kubwa duniani yenye kutofautiana baina ya nchi na nchi. Nchini Marekani kwa mfano haja ya kuwepo kwa utaratibu unaofanana na huu wa kuwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ilionekana katika miaka 1930 kutokana na anguko kubwa la uchumi wa Marekani na dunia lililojulikana kama "The Great Dipression" lilitokea hasa kuanzia 1929 – 1932.

Katika kipindi hicho, Marekani ilishuhudia umasikini uliokithiri hasa kwa wazee waliokuwa wameshastaafu, watu waliopoteza ajira, wanawake wasio na waume, mayatima na watoto waliokuwa hawaishi na familia zao. Kuanzishwa kwa utaratibu wa Hifadhi ya Jamii kulionekana kuwa ni jambo la lazima katika Taifa hilo na hivyo Sheria ya Hifadhi ya Jamii ilitungwa na kuanza kufanya kazi baada ya kusainiwa na Rais wa 32 wa nchi hiyo Franklin Rooselvet tarehe 14, Agosti, 1935.

Haja ya kuwa na Hifadhi ya Jamii ilipata nguvu duniani baada ya tangazo la Umoja wa Mataifa la mwaka 1948, lililotilia mkazo juu ya umuhimu wa nchi duniani kuandaa utaratibu unaohakikisha kuwepo kwa hifadhi ya jamii, ili kulinda maslahi ya makundi mbali mbali. Utekelezaji wa agizo hilo ulipelekea kuundwa kwa Azimio la Shirika la Kazi Duniani nambari 102 la Hifadhi ya Jamii la mwaka 1952.

Baada ya hapo, nchi mbali mbali zilianzisha utaratibu wa kuwa na hifadhi ya jamii kwa mifumo tofauti. Hivyo, Hifadhi ya Jamii ni dhana pana na imekusanya mambo mengi. Hata hivyo, moja ya tafsiri tunayoweza kuipa ni kuwa Hifadhi ya Jamii ni maandalizi au kinga ya kiuchumi na kijamii anayowekewa mwananchi ili aweze kuwa na kinga ya kipato katika nyakati tofauti za umri wake.

Kwa upande wa Zanzibar, utaratibu wa kuwa na Hifadhi ya Jamii vile vile una hisotria ndefu. Utaratibu huu ulikuwepo kabla ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Hata hivyo, walionufaika wakati huo ni wakoloni wenyewe na wanyonge wachache ambao walibahatika kufanya kazi za ukarani katika Serikali ya Kikoloni.

Mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya 1964, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilifanya jitihada kubwa katika kuanzisha Hifadhi ya Jamii kwa wananchi wake kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali. Mfumo huu ulikuwa ndiyo njia kuu ya Hifadhi ya Jamii hapa Zanzibar mpaka mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Kutokana na mabadiliko mbali mbali ya kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na ongezeko la idadi ya watu, ilionekana haja ya kuwa na mfumo ulio bora unaokidhi na kwenda sambamba na mabadiliko yaliyotokea.

Kwa hivyo, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar tunaoendelea nao hivi sasa ulianzishwa kwa Sheria Na.2 ya mwaka 1998 ambayo ilirekebishwa na Sheria Na. 9 ya mwaka 2000. Vile vile, Sheria hii nayo ilirekebishwa kwa notisi ya Serikali ya mwaka 2004 na kuanzishwa upya kwa Sheria Na. 2 ya mwaka 2005 baada ya kufanyiwa mapitio makubwa. Juhudi hizi ndizo zilizopelekea kuwa na mfumo bora tulio nao hivi sasa ambao unaendelea kuimarika na kupendwa na wananchi siku hadi siku.

Inaleta faraja sana kufahamu kwamba, mfumo wa kujichangia kwa hiari unatoa fursa kwa wanachama kunufaisha watoto wao kwa mafao ya elimu. Mwanachama anapata fursa ya kumsajili mtoto na kumchangia mafao ya elimu ili yaweze kumsaidia mtoto wake wakati wa kujiendeleza katika elimu ya juu. Utaratibu huu utatoa fursa ya pekee kwa wazee wenye dhamira njema ya kuwekeza kwa maendeleo ya elimu ya watoto wao.

Uzinduzi wa Mfumo wa kujichangia kwa hiari na mfumo wa ZSSF wa kutoa fao la uzazi, kwa maana ya kwamba kinamama wanaokwenda kujifungua watakuwa wanalipwa na ZSSF, ni hatua muhimu sana ya kutekeleza kwa vitendo agizo la Shirika la Kazi Duniani -ILO lisemalo "Hifadhi ya Jamii kwa wote" (Social Protection for All).

Uamuzi huu wa kutoa fao la uzazi unakwenda sambamba na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuimarisha ustawi wa kinamama wajawazito pamoja kupunguza vifo vya watoto ambavyo baadhi ya wakati husababishwa na umasikini unaopelekea watoto kufa kabla ya kuzaliwa, kukosa mahitaji ya msingi kwa afya zao au huduma muhimu wakati wanapozaliwa na mara baada ya kuzaliwa.

Kuanzishwa kwa Mifuko ya aina hii kunatoa fursa nzuri kwa wananchi wengi wa Unguja na Pemba, mashamba na mijini, walio katika sekta zisizo rasmi ya kuweza kujiwekea kinga ya kipato ambayo itakuwa na umuhimu mkubwa hasa kwa maisha yao ya uzeeni.

Hata hivyo, ili wananchi waweze kuzitumia na kunufaika na fursa hizi mpya, ni vyema kwa uongozi wa ZSSF kuongeza kasi ya utoaji wa elimu juu ya namna ambavyo wananchi wanaweza kujiunga katika mfumo huu mpya wa kuchangia kwa hiari, pamoja na fursa watakazoweza kunufaika nazo, hasa suala hili la kuweza kupata mafao kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya watoto wa wachangiaji.

Akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa wadau wa ZSSF katika ukumbi wa Salama - hoteli ya Bwawani Zanzibar, Dk. Shein ameiagiza ZSFF kufanya kazi kwa karibu na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma katika utoaji wa elimu kwa wananchi walio katika ajira zisizo rasmi, akiamini kuwa mashirikiano kati ya ZSSF na Wizara hizo mbili yatarahisisha kuwafikia na kuwapata wananchi wanaojishughulisha na sekta zisizo rasmi pamoja na vikundi mbali mbali vya ujasiriamali vilivyopo nchini.

"Ni muhimu kuzingatia kwamba kundi kubwa la wananchi ni lile la wanaojishughulisha na ajira zisizo rasmi. Imani yangu ni kuwa wananchi watachangamkia fursa ya kujiunga na Mfumo wa kujichangia kwa hiari ili waweze kujiwekea hazina iliyo muhimu hasa kwa maisha ya uzeeni". Alisema Dk. Shein.

Vile vile ili kufanikisha hatua hii, waajiri wana wajibu mkubwa wa kujisajili kama ni wanachama wachangiaji na kuwasajili wafanyakazi wao kama ni wanachama wanufaika wa ZSSF. Hivyo ni vyema waajiri binafsi wakahakikisha wanawasilisha michango kwa wakati ili kurahisisha shughuli za uendeshaji wa taasisi hii na kujenga misingi mizuri kwa wafanyakazi wao wakati wanapostaafu. Wafanyakazi hasa katika sekta binafsi lazima wahakikishe kuwa waajiri wao wanawasilisha michango kwa mujibu wa viwango na taratibu zilizopo kisheria.

# Dk. Shein azindua mbio za mwenge Songea


*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akisalimiana na viongozi mara alipowasili katika Uwanja wa Maji maji Songea Mkoani Ruvuma tarehe 29 Aprili, 2015*

Uzinduzi wa mbio za mwenge ambao hufanyika kila mwaka tokea ulipoanzishwa rasmi na marehemu baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwezi Desemba 9, mwaka 1961 katika Milima Kilimanjaro, limekuwa jambo lenye manufaa makubwa kwa Watanzania kutokana na mafanikio yanayotokana na mchango wa mwenge huo.

Mchango wa mwenge unajidhihirisha wazi, kwani mbio hizo zimewezesha kuanzishwa kwa miradi mingi ya kijamii nchi nzima. Kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya Tanzania Bara, mwaka 1961 hadi mwaka 1998, miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 15 iliweza kuzinduliwa, na tokea mwaka 1998 hadi sasa, miradi mingine ya zaidi ya shilingi bilioni 80 imezinduliwa.

Viongozi wakuu wa Serikali wamekuwa wakiitumia fursa ya kuzindua mbio za mwenge kutoa maelekezo muhimu yenye mnasaba na mwenendo wa maisha ya jamii na maendeleo ya nchi kwa jumla.

Akizindua mbio za mwenge kwa mwaka huu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alizungumzia Suala la Uchaguzi Mkuu ambalo ni muhimu kwa wananchi wote wa Tanzania, huku akiwataka wananchi kuitumia haki yao hiyo ya kidemokrasia kwa kushiriki kwa amani katika mchakato mzima wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na kujiandikisha.

Aliwataka wananchi kutambua kuwa kupiga kura ni nafasi pekee ya kuwachagua viongozi watakaowaongoza katika jitihada za kujenga Tanzania inayoendelea kuimarika zaidi katika sekta zote muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kisiasa na katika nyanja ya sayansi na teknolojia.

Dk. Shein alizungumzia kwa upana suala wananchi kujiepusha na mambo yote yanayoweza kuleta mitafaruku wakati na baada ya uchaguzi, pamoja na aina zote za udanganyifu ili uchaguzi uweze kuwa huru na wa haki na kuendelea kuidhihirishia dunia namna Tanzania ilivyokomaa kisiasa na kuendelea kuwa nchi ya kupigiwa mfano.

Dk. Shein alitumia fursa hiyo kulizungumzia suala la rushwa ambalo limekuwa likiongelewa mara nyingi na athari zake zinajulikana. Rushwa huchangia kwa kiwango kikubwa kuwanyima wananchi haki zao za msingi kama vile matibabu, elimu, makaazi na heshima ya utu wao.

Alisema katika wakati huu ambapo nchi inaelekea kwenye uchaguzi mkuu, kila mtu ana wajibu wa kufahamu kuwa rushwa inadhoofisha maana ya uwakilishi, kwa sababu wale wanaochaguliwa kwa njia za rushwa huwa hawana ridhaa kamili ya wapiga kura. Ni sahihi kusema kuwa uwakilishi wao ni batili.

"Viongozi ambao huchaguliwa kwa rushwa watakuwa wamevaa nembo ya rushwa, daima kwao haitokuwa rahisi kuwa mstari wa mbele kusimamia mapambano dhidi ya rushwa yanayoendelezwa na Serikali zetu zote mbili na yanayoungwa mkono na wananchi". Alisema

Suala jengine ambalo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amelikemea vikali ni ubadhirifu wa mali ya umma kwa kujilimbikizia mali, jambo ambalo alisema haliwezi kuleta tija katika Tanzania ya leo.

"Napenda kuchukua fursa hii kuzidi kuwahimiza Watanzania wenzangu kukataa kutoa au kupokea rushwa na kuwa tayari na wepesi wa kutoa taarifa za rushwa kwa vyombo vinavyohusika na kwa kuzingatia kanuni, taratibu, maadili na sheria zilizopo. Hatuwezi kuijenga nchi yetu kwa kasi tunayoitaka ikiwa tutajenga utamadaduni wa kuogopana" alisema.

Suala la mshikamano miongoni mwa Watanzania pamoja na kuimarisha Muungano vile vile ni suala lililokuwa limebeba uzito maalum kwenye hotuba ya Rais wa Zanzibar katika sherehe za uzinduzi wa mbio za mwenge mwaka huu, akitahadharisha kundi la baadhi ya watu walioibuka na kujaribu kutaka kuwagawa Watanzania kwa misingi ya udini, ukabila, itikadi za kisiasa na hata matabaka ya kiuchumi na kijamii.

"Wakati tunazindua Mbio za Mwenge wa Uhuru leo hii, nashauri kila Mtanzania akae chini na kujiuliza; kama taifa letu, kwa bahati mbaya likigawanyika tutafaidika kwa lipi" alihoji Dk. Shein.

Amesisitiza haja ya kuendelea kutumia Mbio za Mwenge wa Uhuru kulinda umoja wa kitaifa, kila mahali utakapopita ulete matumaini mapya kwa kuhimiza amani na upendo miongoni mwa Watanzania.

# Wanawake wa Zanzibar waadhimisha siku yao

## ■ Wataka jitihada za kuwaendeleza wanawake ziendelee kufanywa



*Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mama Mwanamwema Shein, akiangalia bidhaa zinazozalishwa na Wanawake Wajasiriamali wa Kikundi cha Sanaa cha Maigizo wakati wa maonesho ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani yalioandaliwa na Kikundi cha "Zanzibalicious Women Group" yaliofanyika viwanja vya hoteli ya Bwawani Zanzibar tarehe 21 Aprili, 2015*

Kila ifikapo tarehe 8 Machi ya kila mwaka wanawake wa Zanzibar huungana na wanawake wengine Duniani kote kuadhimisha siku yao maalum kwa lengo la kufikiria njia bora zaidi zitakazosaidia kuzipatia ufumbuzi changamoto mbali mbali zinazowakabili katika maisha yao ya kila siku kijamii, kiuchumi na kimaendeleo.

Tarehe 8 Machi imeidhinishwa rasmi na Umoja wa Mataifa mwaka 1977 kuwa siku ya wanawake duniani kwa lengo la kutathmini haki, maendeleo na masuala ya usawa wa kijinsia pamoja na changamoto zinazowakabili wanawake katika kila pembe ya Dunia.

Kwa upande wa Zanzibar kwa mwaka huu, siku hii iliadhimishwa tarehe 22 Machi katika Hoteli ya Bwawani Zanzibar na Umoja wa Wanawake wanaoishi Zanzibar (Zanzibalicious) ambao wameweza kupiga hatua kubwa za kimaendeleo. Jumuiya hii iliweza kuungana na Jumuiya ya Kimataifa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuadhimisha siku hii kwa upande wa Zanzibar ikiwa na kauli mbiu isemayo 'Hamasisha Hatua Madhubuti Kumuendeleza na Kumtambua Mwanamke'.

Taasisi ya Zanzibalicious iliona upo umuhimu wa kuwasaidia wanawake ambao bado hawajajikwamua kiuchumi kwa kuunga mkono juhudi zinazochukuliwa na Serikali kufikia dhamira yake ya kupunguza umasikini na kuwawezesha kukabiliana na changamoto ambazo zinawakwaza wanawake katika harakati za maisha yao ya kila siku.

Umoja huo umeweza kupata mafanikio mbali mbali ikiwemo kuwapa elimu na kuwawezesha wanawake kuunda vikundi vidogo vidogo vya maendeleo kwa kuanzisha miradi tofauti ambapo mafanikio ya wazi yameweza kuonekana kwa kinamama wa Chaani na Matemwe.

Vile vile Zanzibalicious imeweza kutoa misaada ya hali na mali kwa waathirika wa dawa za kulevya ikiwa ni moja ya kumkwamua mwanamke pamoja na kutoa misaada mingine mingi kwa wanawake wasiojiweza ikiwemo hospitali kuu ya Mnazi Mmoja na kuwasaidia kinamama wajane.

Pamoja na mafanikio hayo umoja huu umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo jamii yenyewe kutokujua changamoto inazokabiliana nazo. Kwa mfano siyo wengi miongoni mwa wanawake wanaofahamu kwa undani au wanaokerwa na athari za ndoa za utotoni, ukatili wa kijinsia na kuwepo kwa mfumo dume, mambo ambayo yamekuwa yakiongezeka sana ndani ya jamii ambamo wanawake wenyewe



*Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mama Mwanamwema Shein akizindua Mfuko wa Wanawake wa "Zanzibaliciuos Women Group" kwa kuchangia shilingi milioni tano wakati wa chakula cha mchana kilichoandaliwa kwa ajili ya kuchangia mfuko huo tarehe 21 Aprili, 2015*

wamekuwa mashuhuda.

Lakini kwa upande mwengine tatizo la fedha nalo limeonekana kuwa ni kikwazo cha kuwawezesha wachache wenye uelewa mpana wa mambo hayo kuweza kuwafika wanawake wanaoishi katika mazingira magumu na kuwasaidia kuondokana na hali hiyo duni ambayo haikubaliki.

Katika jitihada za kuunga mkono juhudi za "Zanzibarlicious", Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo muda wote imekuwa ikitoa kipaumbele maalum katika masuala yote yanayowahusu wanawake, imeona haina budi kupitia kwa wake wa viongozi wa Serikali, kuunga mkono juhudi za taasisi hiyo kwa njia tofauti, ikiwa ni pamoja na kuitisha harambee itakayowezesha kupata fedha za kusaidia uendeshaji wa shughuli za taasisi hiyo.

Wake hao wa Viongozi wakiongozwa na Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Mama Mwanamwema Shein, kwa kushirikiana na "Zanzibalicious" wameuzindua rasmi umoja wao pamoja na kuendesha harambee kwa ajili ya kuchangia umoja huo. Mama Shein aliweza kuwa mfano kwa kuchangia shilingi milioni tano (5,000,000/=) kwa ajili ya kusaidia "Zanzibalicious" kufikia malengo yake ya kuwasaidia kinamama wengine.

Juhudi zinazochukuliwa na "Zanzibalicious" za kumuinua mwanamke kiuchumi ni kuunga mkono azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein za kuwawezesha wananchi kiuchumi pamoja na utekelezaji wa mikakati ya udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa vijana na watoto.

Katika hafla hiyo Mheshimiwa Mama Mwanamwema Shein alitoa wito kwa Umoja huo kuongeza jitihada zao katika kushirikiana na taasisi za Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi na ustawi wa jamii.

Amesema yeye binafsi akiwa Mlezi wa Umoja wa Wake wa Viongozi wa CCM pamoja na Mwenyekiti wa Umoja huo Mama Asha Suleiman Iddi wameridhika kuona kwamba malengo ya Umoja wa Wanawake wa "Zanzibalicious" yanalingana na yale ya Umoja wao, hasa katika suala la kuwasaidia vijana na wanawake kujiendeleza kiuchumi. Hivyo, mama Shein alishauri kwa vikundi hivyo viwili kuunganisha nguvu zao ili kuweza kutoa msukumo mkubwa zaidi katika kuwasaidia wananawake na kukuza ustawi wa jamii na nchi kwa jumla.

Mama Shein alisisitiza umuhimu wa kuwazingatia zaidi kinamama ambao wanaishi vijijini pamoja na wenye mahitaji maalum kwa kuwa mara nyingi wamekuwa wakisahauliwa na hivyo kukosa fursa muhimu katika kujiletea maendeleo yao.

Vile vile, Mama Mwanamwema Shein alisema kuwa jamii ina wajibu wa kushirikiana na Serikali katika kampeni ya kupiga vita ukatili dhidi ya wananwake na watoto na vitendo vyote vya udhalilishaji wa kijinsia.

"Tutoe ushirikiano kwa vyombo vya sheria na tuzidi kuimarisha malezi mema kwa watoto wetu kwa mujibu wa maadili yetu" alisisitiza Mama Shein.

Mama Mwanamwema Shein alimalizia kwa kutoa wito kwa wanawake kuwa waendelee kuwa wamoja katika kufanikisha masuala ya maendeleo. "Sisi ni jeshi kubwa, tushikamane na jamii yetu itashikamana na kupiga hatua kubwa ya maendeleo" alisema Mama Shein.

Katika kukabiliana na changamoto za wanawake Mheshimiwa Mama Shein amekua akichukua juhudi kubwa ambazo hazinabudi kuendelezwa na kungwa mkono na wanajamii ili kuweza kumpatia maendeleo mwanamke wa Zanzibar, kwani utafiti uliofanywa na "Zanzibalicious" umeonesha kuwa bado wapo wanawake Zanzibar wanaoishi katika mazingira duni ya umasikini kwa kutojitambua na kukosa elimu ya uelewa jinsi ya kukabiliana na mazingira waliyomo.

# Msaada wa Vyarahani utawasaidia kinamama



*Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mama Mwanamwema Shein akizungumza na Balozi Mdogo wa China Bibi Wu Yan kabla ya kukabidhi msaada wa vyerahani katika hafla iliyofanyika Ikulu ya Migombani tarehe 24 Machi, 2015*

Wakati ushirikiano na uhusiano wa kindugu baina ya Zanzibar na China ukiendelea kuimarika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ile ya Jamhuri ya Watu wa China zinaendelea kupanua wigo wa misaada yake kwa jamii kwa kuweka kipaumbele kwa wananchi walioko vijijini.

Hayo yamedhihirika pale Mke wa balozi Mdogo wa China aliyepo Zanzibar Bi Wu Yan alipokabidhi vyarahani 10 kwa Mheshimiwa Mama Mwanamwema Shein – Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa niaba ya kikundi cha kinamama wake wa viongozi ili waweze kuvifikisha vyarahani hivyo kwa walengwa ambao ni vikundi vya wanawake wajasiriamali katika maeneo mbali mbali vijijini.

Sherehe hiyo ya kukabidhi vyarahani ambayo ilifanyika Ikulu ya Migombani Zanzibar kwa niaba ya Ubalozi Mdogo wa China uliopo Zanzibar kwa ajili ya kuwasaidia wanawake waliopo vijijini, ni muendelezo wa misaada mbali mbali inayotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa wanawake na wananchi wote wa Zanzibar kwa jumla.

Hatua hiyo inatokana na ukaribu uliopo baina ya Bi Wu Yan na Mheshimiwa Mama Mwanamwema Shein pamoja na kikundi cha wake wa Viongozi kuwa nae karibu katika ziara zao wanapokwenda vijijini na kuwasaidia wanawake kuweza kujikwamua na umaskini sambamba na kusherehekea siku ya wanawake Duniani ambayo hufanyika kila mwaka mwezi wa Machi.

Bi Wu Yan alimueleza Mama Mwanamwema Shein na wake wa

viongozi hao kuwa, wanawake wa Zanzibar wamekuwa mstari wa mbele kushiriki katika mambo yote muhimu ya kuleta maendeleo.

Alisema kuwa Wazanzibari wameweza kujishughulisha zaidi katika kazi za mikono hivyo anaamini vyarahani hivyo vitaweza kusaidia kuzidisha kasi ya maendeleo kwa wanawake hao wa vijijini.

Vile vile Bi Wu Yan alisema kuwa amevutiwa sana na juhudi zinazochukuliwa na kikundi cha wake wa viongozi kinachoongozwa na Mama Mwanamwema Shein za kuwapatia wanawake maendeleo hasa wale wa vijijini. Hivyo ameamua kushirikiana na kikundi hicho ili kuendeleza juhudi zao na vile vile kuzidisha ushirikiano na urafiki uliopo baina ya China na Zanzibar.

Vyarahani hivyo 10 vitaweza kuwasidia wanawake pamoja na vijana katika kujiajiri wenyewe hii ikiwa ni katika utekelezaji wa azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein ya kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira hasa kwa vijana kwa kuweza kuwatafutia elimu na njia mbadala za kujiajiri wenyewe.

Akitekeleza azma hiyo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba, Mama Mwanamwema Shein alisema kuwa msaada huo umekuja wakati muafaka na vyarahani hivyo vitagaiwa kwa wanawake wenye mahitaji hayo ili viweze kutumika vizuri na kuleta manufaa kwa jamii.

Mama Shein alitoa shukurani zake za dhati kwa Balozi mdogo wa China aliopo Zanzibar Mheshimiwa Xie Yunliang kwa kuweza kuisadia Zanzibar kwa kushirikiana na Bi Wu Yan Zanzibar imeweza kupiga hatua ya kimaendeleo kupitia michango hiyo wanayoitoa.

Vile vile, Mama Mwanamwema Shein alisema kuwa vijana wengi wa Kizanzibari wameweza kujiendeleza kielimu nchini China, fursa ambazo ni matokeo ya udugu na urafiki ulioanzishwa na waasisi marehemu Mao Tse Tung na Marehemu Abeid Amani Karume mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964.



*Mke wa Balozi Mdogo wa China akikabidhi vyerahani kwa mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mama Mwanamwema Shein katika hafla iliyofanyika Ikulu ya Migombani tarehe 24 Machi, 2015*

# “Biogas” inavyosaidia maisha ya jamii



*Mtambo wa bioges ulio tayari kwa matumizi*

Mabadiliko katika mfumo wa maisha ya mwanadamu ni suala la lazima siyo tu kimaumbile, lakini vile vile kimazingira, kiufundi na kijiogorafia. Wanasayansi walibainisha kinadharia na baadae kushuhudiwa kivitendo matukio mbali mbali yaliyothibitisha kwamba mabadiliko katika maisha ya mwanadamu ni jambo lisiloepukika.

Kwa kufahamu tu kuwa kimaumbile watu wengi wamekuwa na hofu ya mabadiliko na hivyo kuendelea kulemaa na mambo ambayo wameyazowea, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika matukio tofauti, amekuwa akisisitiza umuhimu wa wananchi kukubali kubadilika kulingana na hali halisi ilivyo sasa. Moja ya jambo hilo ni kuacha kufanya kazi kwa mazowea.

Hali ya mabadiliko ya tabianchi duniani kote, yanatoa indhari kubwa kwa jamii kujiweka tayari na kuchukua kila hatua ya tahadhari inayowezekana kwa lengo la kukabiliana na changamoto zinazopelekea hali hiyo, ambayo imekuwa tishio kubwa kwa maendeleo ya uchumi na maisha ya wanadamu na viumbe wote duniani.

Wapo miongoni mwetu wanaofikiria kwamba uchumi na mazingira ni masuala mawili tofauti, ambayo harakati za kuyafikia malengo ya suala moja huathiri vibaya uwezekano wa kufanikisha



*Taa ya Biogesi*

malengo ya suala jengine. Uchumi na Mazingira unahimiza mabadiliko ya mifumo ili kutambua kuwa mahitaji ya kimaumbile kwa maisha ya binadamu, yanaweza kufikiwa kwa pamoja.

Ukuaji wa uchumi unaozingatia matumizi yasiyo endelevu ya maliasili hauna manufaa katika dunia ya leo, hivyo watu wanapaswa kubadilika kwa kuachana na mbinu za kizamani za ukuaji wa uchumi wa matumizi shinikizi ya rasilimali, ambapo maendeleo yamekuwa yakigharimu mazingira, badala yake, wanapaswa kufuata mbinu mpya ambazo tija huongezwa kwa kutumia na kusimamia maliasili kwa ufanisi zaidi.

Teknolojia ya kisasa ya matumizi ya gesi mboji ni moja ya aina ya nishati zinazosaidia kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kuzalisha mbolea ya mboji ambayo imethibitishwa kurutubisha udongo.

Biogesi ni gesi inayozalishwa na baktiria wanapovunjavunja malighafi zinazooza kwa urahisi kama vile kinyesi cha ng'ombe na aina nyangine ya mifugo pamoja na mabaki ya jikoni yanapowekwa kwenye sehemu isiyokuwa na hewa ya oksijini. Lakini kwa hapa Zanzibar utengenezaji wa nishati hii inatumiwa kwa kinyesi cha Ng'ombe tu, licha ya kutumiwa kwa aina nyengine ya kinyesi cha wanyama na hata binaadamu.

Uzalishaji wa biogesi hutumia teknolojia rahisi ambapo Mtambo wa biogesi hujumuisha tanki kubwa au mahodhi ambayo hujazwa samadi inayochakachuliwa na bakteria, na matokeo yake ni upatikanaji wa gesi pamoja na mbolea hai.

Mtambo huu huwa na sehemu ya kujazia samadi na mchanganyiko mwingine unaotumika kutengeneza gesi, sehemu ya chujio, ambayo husaidia kukusanya mbolea ambayo imeshachakachuliwa kutoka nje ya mtambo. Mitambo ya biogesi imegawanyika katika makundi matatu kulingana na mahitaji ya mtumiaji na uwezo wa kulisha mtambo.

Kuna mtambo wenye mita za ujazo nne, sita, tisa, na kumi na tatu. Mkulima mwenye mtambo wa mita za ujazo sita, atahitaji kuwa na ng'ombe watatu kwa ajili ya kuzalisha malighafi ya mtambo huo. Baada ya mtambo kujengwa, unahitajika kumwagiliwa kwa siku 14 ili kuruhusu kukomaa.

Baada ya hapo, mtumiaji anatakiwa kujaza samadi kwa kipindi cha siku hamsini bila kutumia. Hatua hii inatoa nafasi kwa bakteria kuweza kuchakachua samadi na malighafi nyingine na hatimae kupata gesi.

Hivyo basi wakati umefika kwa Wazanzibari kufukuzia fursa hii adhimu na adimu kwa hapa Zanzibar ili kuongeza idadi ya wazalishaji wa gesi hii ya samadi yenye manufaa kwa maendeleo ya ufugaji, kilimo na uhifadhi wa mazingira nchini.

Makala hii imefanikiwa kuwatembelea baadhi ya wafugajii mahiri na hodari na wenye tunu ya maendeleo katika sekta ya ufugaji. Mmoja kati ya wafugaji hao ni Bwana Suleiman Abdallah wa Kijiji cha Machui Unguja, ambaye ameelezea furaha yake kutokana na mafanikio aliyoyapa baada ya kuanzisha mtambo wa gesi mboji kijijini kwake.



*Matumizi ya Biogesi kwa kupikia husaidia kutunza usafi wakati wa kupika.*

Bwana Suleiman alianza ufugaji wa Ng'ombe mwaka 1996 akiwa na ng'ombe watatu tu ambao wameongezeka hadi kufikia zaidi ya ng'ombe 50 alionao sasa. Ng'ombe hao anawaendesha vyema na wanamletea faida kubwa katika maisha yake ya kila siku.

"Nilipelekwa kwa wafugaji wenzangu katika maeneo ya Fuoni ambao wameanzisha mitambo ya gesi mboji ili kujionea na kujifunza faida za matumizi ya Mitambo hiyo na ndipo nikashawishika na mimi kuanzisha mitambo ya biogesi katika shamba langu la Mifugo Machui". Alielezea kwa shauku kubwa Suleiman.

Suleiman alianza na mtambo mmoja wa gesi mboji ambapo sasa amehamasika na kuongeza mitambo miwili na kutimiza idadi ya mitambo mitatu yenye mita za ujazo 13 ambayo humsaidia kwa kiasi kikubwa katika matumizi yake ya nyumbani kwa kupikia na katika biashara zake za Maziwa .

"Tangu kuanzisha kwa mitambo hii imenisaidia sana katika matumizi yangu ya nyumbani na sasa nimepunguza kwa kiasi kikubwa matumizi ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia katika nyumba zangu mbili na biashara zangu za kuchemsha maziwa ."alisema kwa majigambo Suleiman .

Aidha, ameeleza kuwa malighafi ambayo inapatikana katika mtambo wa gesi mboji hutumika kama mbolea kwa ajili ya kustawisha shamba lake la malisho kwa ajili ya mifugo yake .

Vile vile Bwana Suleiman amesema licha ya kuhamasika katika uanzishaji wa mitambo hiyo ya biogas, anakabiliwa na tatizo la eneo la kufugia kwani amesema eneo la ardhi alilonalo ni dogo sana kiasi ambacho hawezi kulikuza shamba lake la malisho na kujiwekea akiba ya kutosha kwa matumizi katika msimu wa kiangazi.

Vilevile amewahamasisha wafugaji wenzake ambao bado hawajaanzisha mitambo hiyo kuanzisha kwani ina faida kubwa kwa maendeleo bora ya ufugaji wenye mafanikio.

Makala hii iliingia ndani zaidi hadi katika familia ya Bwana Suleiman Abdallah ambapo ilizungumza na mmoja ya wanafamilia hao Bibi Aisha Rajab ambaye nae alielezea mafanikio zaidi anayoyapata katika matumizi ya gesi ya samadi katika mapishi yake.

"Nishati hii husaidia kuokoa muda wa kupika kwani huivisha chakula kwa haraka, na katika mazingira salama tofauti na gesi nyengine " alifafanua Aisha.

Amefahamisha kuwa gesi ya samadi inasaidia kwa kiasi kikubwa katika uhifadhi mazingira tofauti na kuni, mkaa na hata jiko la stima ambayo hutoa moshi mwingi na kupelekea uchafuzi wa mazingira na athari kwa jamii.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Uzalishaji Mifugo Zanzibar Bwana Hafidh Said Baalawy amesema licha ya baadhi ya wafugaji kuhamasika uanzishaji wa mitambo hiyo ya gesi ya samadi gesi mboji lakini idadi bado ni ndogo.

"Mimi nawasihi wafugaji wenye ng'ombe wao mabandani kuanzisha mtambo wa biogas katika maeneo yao ambao unapunguza gharama ya nishati ya kupikia na kuimarisha mazingira na wasiogope gharama ambapo Serikali imekuwa ikiwasaidia kwa asilimia 20". Alieleeza Mkurugenzi Baalawy.

Hata hivyo, amehimiza kuwepo ushirikiano wa karibu baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na taasisi nyengine zenye dhamana na masuala

ya Mazingira, Misitu na Nishati katika kutoa elimu ya kukuza teknolojia hiyo kwa wananchi mbali mbali nchini.

Jumla ya mitambo 35 ya aina ya mahandaki imeanzishwa katika wilaya mbali mbali za Unguja na Pemba na kuwa na mafanikio makubwa kwa wakulima na wafugaji hao nchini.

Pamoja na kuweko changamoto nyingi za kimazingira, mabadiliko ya teknolojia yanayoendelea duniani sambamba na uhaba wa wataalamu, lazima tukubali kubadilisha aina ya maisha tunayoishi na kuhamasisha wananchi juu ya matumizi ya teknolojia mpya hasa zinazosisitiza matumizi ya nishati rafiki wa mazingira katika shughuli za kila siku katika maisha yetu.

Serikali kuu kwa upande wake nayo inaendelea kujiandaa na matumizi ya gesi asili kwa kupikia na matumizi mengine kwa lengo la kupunguza uzalishaji wa gesi mkaa kwa kiasi kikubwa na kunusuru misitu .



*Fundi kutoka Idara ya Uzalishaji Mifugo akijenga mmoja kati ya mitambo ya biogesi iliopo kisiwani Unguja*



*Jiko la Biogesi*

# Sherehe za Mei Mosi kufanyika Pemba

Maadhimisho ya Sherehe za Wafanyakazi Zanzibar yanafanyika Kisiwani Pemba mwaka huu ambapo wafanyakazi wa Zanzibar wanajumuika na wafanyakazi wengine wa Tanzania na duniani kote kuadhimisha siku hiyo.

Siku ya wafanyakazi duniani inawakumbusha wafanyakazi na watu wote duniani harakati na jitihada za wafanyakazi katika kuchangia maendeleo ya mataifa yao. Historia inatukumbusha kuwa siku hii imetokana na harakati za wafanyakazi huko Chicago nchini Marekani kudai haki zao miaka kadhaa iliyopita.

Hata hivyo, hali katika miaka ya hivi karibuni imebadilika na wafanyakazi huitumia siku hii mahsusi kufanya tathmini ya maendeleo ya wafanyakazi pamoja na changamoto zinazowakabili.

Wafanyakazi wa Zanzibar wanahudhuria kwenye sherehe hizi wakiwa wenye faraja kubwa kutokana na Serikali yao kuchukua hatua mbali mbali za kuboresha maslahi yao katika nyanja zote.

Katika kipindi kisichozidi miaka mitano wameweza kushuhudia Serikali yao inavyozingatia ujumbe wa maadhimisho ya mwaka huu usemao, “Utawala Bora Uzingatie Haki za Wafanyakazi”, jambo ambalo limefanywa kwa umakini mkubwa na Serikali kwa kuundwa taasisi za kusimamia utawala bora na kuzipa mamlaka ya kusimamia haki za wananchi wakiwemo wafanyakazi.

Aidha, kwa namna mbali mbali Serikali imekuwa ikichukuwa hatua za kuyaimarisha maslahi ya wafanyazi na kuchukua hatua nyengine kwa lengo la kuzilinda haki zao.

Wakati huu wafanyakazi wanaposherehekea siku yao ya wafanyakazi duniani, bado wanakumbuka mafanikio makubwa waliyoyapata katika maadhimisho ya Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni jambo lililo wazi kuwa wafanyakazi wa Zanzibar walitoa mchango mkubwa katika kuzifanikisha sherehe hizo ambazo zilikuwa za aina yake.

